

**TMA:** Joto kali kupungua ndani ya mwezi huu

UKURASA 3

**DIWANI** mstaafu auawa kwa mkuki na wafugaji porini

UKURASA 3



**MAUAJI** ya kiongozi wa Hamas Beirut yazidisha shaka ya vita

UKURASA 19

**GAMONDI SASA HATANII, ALITAKA MAPINDUZI CUP**

UKURASA 24

Alhamisi Januari 4, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581545

www.ippmedia.com

LIKE & FOLLOW US
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper

## ALIYECHOMWA VISU 25

# Mbunge aibua mapya utata wa kifo chake



UKURASA 4



Jenista Mhagama

"Tuweke mbele uzalendo na kutoa maoni yatakayosaidia kupatikana sheria bora za kuimarisha mfumo wa vyama vya siasa na demokrsia nchini kwa njia ya maridhiano"



Stephen Wassira

"Mfumo wa vyama vingi si tiketi ya kushamiri uhasama kati ya chama kimoja na kingine"



Salum Mwalimu

"Rais Samia alileta R nne kwa sababu wakati akingia madarakani, nchi ilikuwa katika mtikisiko wa kidemokrasia, uchumi na kijamii"



Gertrude Mongella

"R nne za Rais Samia ni msingi utaokaisaidia taifa katika kipindi hiki cha kutengeneza Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050"



Ado Shaibu

"Kuna mambo yanayoweza kusubiri, lakini si Katiba Mpya. Mchakato wake unatakiwa uanze mara moja ili usaidie katika Uchaguzi Mkuu"

# Waziri: Maoni ya vyama siasa yasichakachuliwe

UKURASA 2

UKURASA WA 5

### KAMATI YAUNDWA KUCHUNGUZA KIFO MJAMZITO

UONGOZI wilayani Kahama, mkoani Shinyanga umeunda timu maalum itakayochunguza kifo cha mjamzito Rachel William (19), aliyefariki dunia Desemba 28, mwaka jana...

UKURASA WA 9

### UHABA WA SUKARI WAIKUMBA MIKOA YA KASKAZINI

SERIKALI imesema uhaba wa sukari ulioikumba mikoa ya Kanda ya Kaskazini ya Kilimanjaro, Arusha, Manyara na Tanga unatokana na Kiwanda cha Sukari cha TPC...

UKURASA WA 24

### KRAMO AREJEA, WATATU WAPYA WAJA SIMBA



KIUNGO wa Simba ambaye alikuwa majeruhi kwa muda mrefu, Aubin Kramo, amerejea nchini akiwa fiti na kujiunga moja kwa moja na kikosi cha timu...

## Mabingwa waibua yaliyojificha kuhusu ugumba kinamama

UKURASA 11

**MICHEZO** AZAM FC YATINGA ROBO FAINALI MAPINDUZI CUP, VITAL'O YAAGA UK. 23

**KATUNI** UK. 6

# Waziri: Maoni ya vyama siasa yasichakachuliwe

**Na Waandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema miongoni mwa mageuzi muhimu yanayohitajika nchini ni kujenga misingi bora ya uwajibikaji katika ngazi mbalimbali za utendaji.

Wakati Makamu wa Rais akielekeza hayo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu, Jenista Mhagama, ameonya uchakachuaji wa maoni yanayotolewa na vyama vya siasa, akiagiza yawasilishwe katika mamlaka husika bila kuchakachuliwa.

Othman aliagiza hayo jana katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNICC) alipofungua mkutano wa siku moja wa wadau Baraza la Vyama vya Siasa katika Jitihada za Kuimarisha Demokrsaia Tanzania.

Alisema hatua hiyo ni muhimu na inahitajika nchini kutokana na kulegalega kwa uwajibikaji katika taasisi mbalimbali za uongozi, siasa, demokrasia, serikalini, Bunge na vyombo vya utoaji haki.

Makamu wa Rais aliitaja ni hatua inayosababisha kuwapo malalamiko kutoka kwa viongozi na hata wananchi wa kawaida.

Othman alisema kwamba iwapo nchi inahitaji kufanya mageuzi, ni muhimu juhudi kubwa zikaelekezwa katika mfumo wa uchaguzi.

Kwa mujibu wa kiongozi huyo, hatua hiyo inahitajika kutokana na ukweli kwamba uchaguzi ndio unaozaa viongozi wa kitaifa na utendaji wa taasisi zote walioaminiwa na wananchi.

"Iwapo taifa litakuwa na viongozi ambao hawatokani na sauti za wananchi, lakini wanatokana na udhaifu wa mfumo uliopo wa uchaguzi, ni ngumu kutarajia kwamba taifa litaweza kujenga uwajibikaji," alisema.

Othman aliwataka washiriki kuwa na dhamira ya dhati ili isaidie mkutano huo kuwa na mjadala utakaosaidia nchi kufikia malengo kwa pamoja na kuwa na sheria zilizowashirikisha wadau wote katika kufanikisha dhana ya mageuzi.

Pia aliwataka washiriki kulitendea haki taifa kwa kuitumia fursa hiyo kwa kutoa michango bora itakayosaidia kuimarisha sheria zinazokusudiwa kutungwa na kufanyiwa marekebisho kwa faida ya taifa.

Alisema Watanzania wamekuwa kila siku wanazungumzia suala la amani na utulivu na nchi kuonekana mfano bora kwa majirani na kwingineko duniani, lakini taifa linapaswa kukumbuka kusimamia haki za watu wote kwa vile msingi wa amani ni haki.

Alisema kuwa hilo linawezekana kutokana na kuwapo sheria bora na taasisi imara na sheria zinazokwenda sambamba na mazingira ya kimahitaji kwa wananchi.

Akizungumzia maono ya R nne za Rais Samia Suluhu Hassan, Othman alisema R ya Reforms (mageuzi) inapaswa kuwa R mama na kama ikitekelezwa kwa dhati na weledi, utekelezaji wa R nyingine tatu (Reconciliation, Rebuilding and Resilience) utakuwa mwepesi.

"Miongoni mwa mageuzi muhimu ambayo nchi yetu inahitaji bila kuchelewa ni kujenga misingi ya uwajibikaji katika ngazi zote. Moja katika ya maradhi yanayolitafuna Taifa letu ni kulegalega kwa uwajibikaji katika ngazi na daraja zote," alisema.

Alisema kulegalega kwa uwajibikaji kumefanya kila mtu alalamike kuanzia kiongozi wa juu kabisa hadi mwananchi wa kawaida.

"Athari yake ni kubwa sana, bila shaka kama tunataka kufanya mageuzi katika suala la uwajibikaji hatuna budi kufanya mageuzi katika mfumo wetu wa uchaguzi, uchaguzi ndio unaozaa uongozi wa kitaifa na utendaji wa taasisi zote," alisema.

Kuhusu maoni ya watu wengi kuhusu jopo la uteuzi wa Tume ya Uchaguzi kuwa na viongozi wa kisiasa na uwakilishi, alisema ni jambo linalowezekana kwa kujadiliana namna bora ya kupata jopo bila ya viongozi wa kisiasa kutilia shaka.

"Nimesikia kilio cha muda mrefu cha vyama vya siasa kuhusu kanuni ya kukokotoa ruzuku kwa vyama. Hili nalo linawezekana bila kuathiri kiwango cha bajeti ya ruzuku kwa kutekeleza mapendekezo ya Kikosi Kazi kwamba asilimia 10 ya bajeti ya ruzuku igawiwe kwa vyama vyote kwa usawa.

"Haya ni baadhi tu ya mambo wenzangu kwenye serikali zetu yazingatiwe kwa nia ya kufanya maboresho ya miswada husika," alisema.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu, Jenista Mhagama, alisema masuala ya demokrasia yanatekelezwa kwa kuzingatia pande zote za Muungano.

Aliwaomba washiriki wa mkutano huo ulioitishwa na Baraza la Vyama vya Siasa na kukusanya wadau mbalimbali wakiwamo viongozi wa vyama vya siasa, kuhakikisha wanaopewa mamlaka ya kuyaratibu maoni hayo kwenye mkutano, yawasilishwe katika mamlaka husika bila kuchakachuliwa.

Hatua hiyo, Jenista alisema itaisaidia serikali kujifunza masuala mbalimbali kupitia ushauri na maoni yatakayotolewa na wadau kwenye mkutano huo shirikishi.

Aliwataka washiriki hao kuweka mbele uzalendo na kutoa maoni yatakayosaidia kupatikana sheria bora za kuimarisha mfumo wa vyama vya siasa na demokrasia nchini kwa njia ya maridhiano na kujenga ustahimilivu na kuleta mageuzi na mabadiliko chanya ya mfumo wa siasa na demokrasia nchini.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili ya Rais Zanzibar (Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi Zanzibar), Hamza Hassan Juma, alisema kunahitajika jitihada za serikali katika kufanya kazi kwa pamoja na kutoa maoni yatakayosaidia wabunge kuchambua zaidi muswada wa sheria zilizopelekwa bungeni ili kusaidia zaidi nchi.

Alisema kukaa pamoja na kujadili mustakabali wa nchi ni nia njema na ni jambo la kujivunia kwa kuwa wengi duniani wanashindwa kufanya hivyo na kwamba suala hilo litachangia kupatikana ufanisi katika mkutano huo.

Msajili wa Vyama vya Siasa nchini, Jaji Francis Mutungi, alisema mkutano huo ni utekelezaji wa maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan kuhusu mapendekezo yaliyotokana na mikutano ya Baraza la Vyama vya Siasa katika kubadilisha sheria mbalimbali zinazohusu uchaguzi na demokrasia.

**STEPHEN WASSIRA**

Mwanasiasa mkongwe, Stephen Wassira alisema R nne zinalenga kujenga daraja la uhusiano na kudumisha umoja wa kitaifa katika serikali yenye mfumo wa vyama vingi ili kusonga mbele kwa pamoja.

Alisema watu wengi wanaichukulia dhana ya mfumo wa vyama vingi tofauti, wakiamini kuwapo kwake ni tiketi ya kushamiri uhasama kati ya chama kimoja na kingine, jambo ambalo si sahihi.

Alisema ili nchi inufaike na mfumo huo, wadau wote wa maendeleo wakiwamo vyama vya siasa, asasi za kiraia, vyombo vya habari na wananchi wanayo kazi kubwa ya kufanya kuhakikisha utekelezaji wake unatimizwa kwa vitendo.

**GETRUDE MONGELA**

Mwanadiplomasia Getrude Mongela, alisema R nne ni msingi utaokaisaidia taifa katika kipindi hiki cha kutengeneza Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 itakayoiongoza nchi kwa miaka 25.

Pia alisema kuna haja kuiweka misingi hiyo katika lugha itakayoeleweka na kila mtu pamoja na kutoa elimu kwa jamii ili aielewe vizuri.

Katibu Mkuu wa Chama cha 'Alliance For the Democratic Change' (ADC), Doyo Hassan, alimpongeza Rais Samia kwa mfumo huo kwa kuwa amesimamia uhuru wa vyombo vya habari na wa kisiasa. Sasa uhuru wa kujieleza na kutoa maoni umeongezeka.

"Ni kiongozi anayetakiwa kuungwa mkono kwa sababu leo tunarudi katika mifumo ambayo tumeipigania tangu mwaka 2012," alisema.

Naibu Katibu Mkuu Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Zanzibar, Salum Mwalimu, alisema Rais alileta mfumo wa R nne kwa sababu aliona kuna haja ya kuliunganisha taifa kwa sababu wakati anakuwa Rais, aliikuta nchi ikiwa katika mitikisiko ya kidemokrasia, uchumi na kijamii.

Alisema mbali na kuliunganisha taifa, mifumo hiyo pia inalenga kuweka misingi thabiti kwa zilizokuwa changamoto za muda mrefu ili zisijirudie tena, akitolea mfano changamoto za kidemokrasia zilizokuwapo kabla ya serikali ya awamu ya tano.

Akizungumzia ustahimilivu, Katibu Mkuu wa Chama cha ACT Wazalendo, Ado Shaibu, alisema kuna mambo yanayoweza kusubiri, lakini si Katiba Mpya na kusisitiza kuwa mchakato wake unatakiwa uanze mara moja ili usaidie katika kipindi cha Uchaguzi Mkuu.

**USAWA KIJINSIA**

Katika mada ya Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa na Sheria ya Gharama za Uchaguzi wa Mwaka 2023, Mwenyekiti wa TWCP-Ulingo, Dk. Avemaria Semakafu, alisema msimamo wao ni 50 kwa 50 katika nafasi za uongozi na hatua hiyo itaboresha demokrasia nchini.

"Kama nchi yetu inaamini binadamu wote ni sawa, inatakiwa mabadiliko yote yalenge jambo hilo. Tungependa kuona sheria inayotoa miongozo ya kuvunja ubaguzi wa aina yoyote katika ngazi ya siasa.

"Katika muswada tunaona yameletwa mabadiliko lakini bado hayajatugusa. Tulipendekeza kuwa na sheria ambayo itatamka wazi ni jinsi gani vyama vyetu vya siasa vitaweza kuundwa na kuongozwa katika nafasi za juu kwenye vyama vya siasa, tunataka tuone sura ya mwanamke na mwanamume," alisema.

Mwenyekiti wa UWT, Mary Chatanda, alipendekeza sheria itamke wazi katika uteuzi wa wagombea kwenye uchaguzi wa ndani na nje ya chama, kila chama kiteue angalau asilimia 20 ya wagombea wanawake katika nafasi zote na itamke kila chama cha siasa kitatumia asilimia fulani ya ruzuku kuwajengea uwezo wanawake na makundi maalum kushiriki katika uchaguzi.

Kiongozi wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, alishauri ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ikaangalie mapendekezo ya kikosi kazi ambayo yalilenga katika nafasi za ngazi ya juu kama nisita wanawake wawe wawili.

"Katika kifungu cha ruzuku ya vyama vya siasa inatokana na idadi ya kura, wabunge na madiwani na mapendekezo yaliyoletwa yanasema isiwe uchaguzi mkuu iwe pamoja na uchaguzi mdogo, msingi wa ruzuku duniani kote ni uchaguzi mkuu, hapa katikati kulikuwa na wimbi la kuunga mkono juhudi, kulikuwa na uchaguzi mdogo na haukuathiri ruzuku.

"Pendekezo la wadau ni kuweka mfumo wa ruzuku kuvijenga vyama kama taasisi yaani asilimia 10 ya bajeti inayotengwa na serikali igawiwe kwa vyama vyote vyenye usajili wa kudumu kwa usawa na itaondoa vyama kwenye mifuko ya watu," alisema.

Zitto pia alipendekeza katika kuweka usawa wa kijinsia, yawekwe masharti chama kitakachofaidika na mgawo huo ni kile kilicho na uwakilishi wa kijinsia.

***Imeandikwa na Augusta Njoji na Jenifer Gilla**


**KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI**

**ABDALLAH MAHMUDI WAZIRI** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 485 CTF – HAOJUE EXPRESS.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/MTW/MTW/1875/2023.**

**KUPOTEA KWA VYETI**



**AGNESS GERALD** anatangaza kupotea kwa cheti cha Diploma ya uuguzi namba ya kuhitimu **NM.465** kilichotolewa na NACTE Kupitia **MUHIMBILI SCHOOL OF NURSING AND MIDWIFERY** mwaka 2015, Cheti cha kuhitimu ASTASHAHADA YA UUGUZI chenye **NO. 06559.** kilichotolewa na TANGANYIKA MEDICAL TRAINING BOARD kupitia NURSE MIDWIFE mwaka 2010 na ASTASHAHADA YA USINGIZI NA GANZI kilichotolewa na MUHIMBILI NATIONAL HOSPITAL from 1st January 2017 to 31st January 2018.
Taarifa ya Polisi: **DOD/DOD/RB/154405/2022.**

**KUPOTEA KWA VYETI**



**AGNES GERALD** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye Index No. **S0476-0001** kilichotolewa na Baraza la mitihani la Taifa kupitia MWANGAZA SECONDARY SCHOOL mwaka 2007, Nyeti vinne vya kuhutimu mafunzo ya uuguzi na ukunga vyenye No. **52916, 63076,** mwaka 2016 vyenye **No. 31877** na 40816 mwaka 2010 vilivyotolewa na **TANZANIA NURSING AND MIDWIFERY COUNCIL.** Yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Taarifa ya Polisi: **DOD/DOD/RB/154405/2022.**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 28544 OF 2023**

**In the matter of the Estate of the late of the late MABULU NHONYA MALEGAMHENE of Azimio within Dodoma City**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION**

**BY DAUDI MABULU NHONYA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 163)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above- named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 10 Day of 1, 2024

RESIDENT MAGISTRATE

**KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI**

**JEREMIA MTERO MAKESENI** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 846 AMW** aina ya HONDA. Chassis namba **MD221302129.** Engine namba **MD17E1402123.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/ARU/ARU/257/2024.**

HABARI KITAIFA

# Diwani mstaafu auawa kwa kuchomwa mkuki na wafugaji

**Na Jumbe Ismailly,** SINGIDA

ALIYEWAHI kuwa Diwani wa Mwamagembe wilayani Manyoni, mkoani Singida, Yahya Masudi (58), anadaiwa kuuawa na jamii ya wafugaji kwa kuchomwa mkuki bega la kushoto na kukatwa na kitu chenye ncha kali kichwani katika pori la hifadhi lililoko kijijini Mwamagembe alikokuwa anaishi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, Kamishna Msaidizi (ACP) Stella Mutahibirwa, alithibitisha jana kutokea kwa tukio hilo, akibainisha kuwa ukatili huo ulifanywa Desemba 30, mwaka jana.

Alisema wafugaji hao waliomuua diwani huyo mstaafu walitokea mkoani Tabora na walikwenda katika pori hilo kwa nia ya kutafuta malisho ya mifugo na kuingiza zaidi ya ng'ombe 100 kwenye moja ya vitalu vya wawindaji vilivyoko kwenye hifadhi hiyo ambayo hulindwa na walinzi walio chini ya Kijiji cha Mwamagembe.

Kwa mujibu wa Kamanda Stella, baada ya mifugo hiyo kuingizwa hifadhini, walinzi waliikamata na kuizuia kwa lengo la kuwatafuta wahusika ili wakamatwe na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria.

Alisimulia kuwa muda mfupi baada ya kuzuiwa mifugo hiyo, kilitokea kikundi cha wafugaji kinachosadikiwa kutoka katika Kijiji cha Majojolo, Kata ya Kilori, wilayani Sikonge, mkoani Tabora na kulivamia eneo hilo.

Kamanda Mutahibirwa alisema kuwa baada ya kikundi hicho kuvamia eneo lililokuwa linalindwa, kiliwashambulia walinzi kwa silaha za jadi kwa lengo la kuirejesha mifugo yao kwa nguvu, jambo lililosababisha kiongozi wa walinzi hao, Masudi kushambuliwa na kufariki dunia.

"Wafugaji hao walifanikiwa kuichukua mifugo yao na kutokomea kusikojulikana. Kutokana na tukio hilo. Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na raia wema linaendelea na msako kuwatafuta watuhumiwa wote waliohusika na tukio hilo," alisema.

Kamanda Stella alisema mwili wa marehemu umefanyiwa uchunguzi wa kitaalamu na kukabidhiwa kwa ndugu kwa hatua za mazishi.



## TMA: Joto kali kupungua mwezi huu

**Na Faustine Feliciane**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), imesema hali ya joto kali iliyoanza tangu mwezi Novemba, mwaka jana inatarajiwa kupungua mwezi huu wa Januari kutokana na kuwapo kwa vipindi vya mvua vinavyotarajiwa kuendelea kujitokeza katika maeneo mengi nchini.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na TMA, vipindi vya mvua katika maeneo mbali mbali nchini vitasaidia kupunguza hali ya joto kali katika baadhi ya maeneo ya nchi.

Aidha, TMA imeeleza kuwa ongezeko la joto nchini husababishwa na kusogea kwa jua la utosi na upungufu wa mvua unaojitokeza katika maeneo mbalimbali.

"Kwa kawaida vipindi vya jua la utosi nchini hufikia kilele mwishoni mwa mwezi Novemba wakati jua la utosi likiwa linaelekea kusini (Tropiki ya Kaprikoni) na hali hiyo hujirudia tena mwezi Februari wakati jua la utosi likiwa linaelekea Kaskazini (Tropiki ya Kansa), lakini kuwapo kwa vipindi vya mvua tunavyovitarajia ndani ya mwezi huu kutapunguza kwa kiasi kikubwa hali ya joto iliyopo sasa," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Mamlaka hiyo imesema wastani wa ongezeko la joto la dunia katika mwaka wa 2023 ulifikia nyuzi joto 1.40C na ulivunja rekodi na kuwa ni mwaka wenye joto zaidi katika historia ya dunia, ukichagizwa na uwapo wa El-Nino na mabadiliko ya tabianchi.

Kwa Tanzania, tathmini imeonesha pia wastani wa ongezeko la joto kwa mwaka 2023 ulikuwa nyuzi joto 1.00C kwa upande wa Tanzania na pia kuufanya mwaka 2023 kuvunja rekodi na kuwa mwaka wenye joto zaidi katika historia.

"Katika kipindi cha Desemba, 2023 kumekuwapo na ongezeko la joto kwa baadhi ya maeneo nchini hususani nyakati ambazo kumekuwa na vipindi vichache vya mvua."

Hadi Desemba 29, 2023 kituo cha Morogoro kiliripoti kiwango cha juu zaidi cha nyuzi joto 33.9 °C ikiwa ni ongezeko la nyuzi joto 1.3 ikilinganishwa na wastani wa muda mrefu kwa mwezi huo.

Kituo cha Tanga kiliripoti nyuzi joto 33.6 °C Desemba 9 (sawa na ongezeko la nyuzi joto 1.5), Dodoma nyuzi joto 33.5 °C, Desemba 19 (ongezeko la nyuzi joto 2.9), Dar es Salaam nyuzi joto 33.2 °C, Desemba 2 (ongezeko la nyuzi joto 1.2) na Zanzibar nyuzi joto 33.4 C sawa na ongezeko la nyuzi joto 1.6, ikiwa ni viwango vya juu vya joto.

TMA imewataka wananchi kuendelea kufuatilia taarifa za hali ya hewa zinazotolewa kila wakati na kufuata ushauri wa wataalamu katika kipindi hiki cha joto kali na hata wakati wa vipindi vya mvua vinavyotarajiwa mwezi Januari katika maeneo mbalimbali ya nchi.

MuCoBa Bank PLC

"Kwa Maendeleo Yako"

P. O. Box 147, Tel. 026-2772165, Fax 026-2772075
Mafinga, Tanzania.
E-Mail: mucoba@mucobatz.com

**TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA ISHIRINI NA TATU (23) WA WANAHISA WA BENKI YA MUCOBA**

Taarifa inatolewa kwa wanahisa kwamba, Mkutano Mkuu wa Ishirini na Tatu wa Wanahisa utafanyika siku ya Jumamosi tarehe 27 mwezi wa Januari 2024 katika ukumbi wa MAM –uliopo Mafinga Mjini kuanzia saa tatu kamili asubuhi.

**AJENDA YA MKUTANO ITAKUA KAMA IFUATAVYO:**

1. Kufungua Mkutano
2. Kuthibitisha Akidi ya Wajumbe
3. Kuchagua Mwenyekiti wa Mkutano
4. Kuridhia ajenda za Mkutano
5. Kuthibitisha Muhtasari wa kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa 22 wa Wanahisa uliofanyika tarehe 18.12.2021.
6. Kupokea,kujadili na kuridhia utekelezaji wa yatokanayo na Mkutano Mkuu wa 22 wa Wanahisa uliofanyika tarehe 18.12.2021
7. Kupokea na kujadili taarifa ya Mwenyekiti wa bodi ya Wakurugenzi ya Mwaka 2023.
8. Kupokea na kujadili taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za Mwaka unaoishia tarehe 31.12.2022
9. Kupokea na kujadili mapendekezo ya Mkaguzi huru wa hesabu za benki kwa mwaka 2022
10. Kupokea na kujadili gawio kwa mwaka ulioishia tarehe 31.12.2022
11. Kupokea na kuidhinisha pendekezo la Malipo ya wajumbe wa Bodi
12. Kuwasilisha taarifa kuhusu mashauri yahusuyo Benki
13. Kupokea na kuidhinisha uteuzi wa wakaguzi wa nje wa hesabu kwa mwaka 2023
14. Kufunga Mkutano.

Notisi hii imetolewa leo tarehe 04/01/ 2024

**MAMBO YA KUZINGATIA**

1. Mwanahisa anayetarajia kuhudhuria Mkutano huu atatakiwa kufanya hivyo kwa gharama zake mwenyewe.
2. Iwapo Mwanahisa anayeruhusiwa kuhudhuria Mkutano na kupiga kura, atashindwa kwa sababu zozote zile kuhudhuria Mkutano, ataruhusiwa kuchagua Mwakilishi kuhudhuria na kupiga kura kwa niaba yake kwa kufuata na kuzingatia taratibu na sheria za Kampuni.
3. Nakala za Makabrasha ya Mkutano zitapatikana pia kwenye ofisi yetu kuu iliyopo Mafinga- Iringa.

**KWA AGIZO LA BODI YA WAKURUGENZI**
**DENIS RWEYENDERA**
**KATIBU - BODI YA WAKURUGENZI**

21774702



Wafanyabiashara wakiuza bidhaa zao karibu na taka zilizojaa maji machafu yanayotiririka kutoka kwenye taka hizo katika soko la Temeke Stereo jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mkakati kutangaza vivutio vya utalii Kagera wasukwa

**Na Halfani Chusi**

WASANII 100 wa kada tofauti nchini, wanatarajiwa kuzuru mkoani Kagera mwezi ujao kwa lengo la kutangaza vivutio vya utalii vilivyoko mkoani huko ili kuvutia watalii.

Ni mkakati uliotokana na ziara ya mmiliki wa Kampuni ya Sepenga Entertainment, Goodhope Ntimba, maarufu Maadam Sepenga, ametembea mkoa huo na kubaini una vivutio vingi vya utalii, lakini havitangazwi.

Ziara hiyo ya wasanii iliyopewa jina la The Grand Kagera Tour, pia itahusisha wasanii wa kada ya uigizaji ambao wanatarajiwa kuandaa igizo litakalooneshwa kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii, likibeba maudhui ya mila na destruri za wakazi wa Kagera.

Msemaji wa The Grand Kagera Tour ambaye ni mwigizaji, Jafari Makatu, alibainisha katika mazungumzo na Nipashe mwezi uliopita mkoani Dar es Salam kuwa, Maadam Sepenga alizunguka maeneo mengi mkoani Kagera kwa miaka ya minne kwa gharama zake kujionea vivutio vya utalii.

Alisema kuwa Maadam Sepenga baada ya ziara hiyo, aliamua kuwashirikisha wasanii wengine kuungana naye kutangaza vivutio vya utalii vilivyoko Kagera.

Alisema vivutio vilivyoko katika mkoa huo vinajumuisha mabaki ya mapango yaliyokuwa yanatumiwa na machifu; watu walikuwa wanayatumia kuabudu na kufanya ibada za mavuno.

"Kwa sababu kule kuna mila mbalimbali, kwa mfano Chifu Manyika aliacha nyayo zake, hivyo ni vitu ambavyo vinaweza kuiingizia mapato serikali.

"Kuna mto mmoja unatiririsha maji yanapotoka juu yanakuwa ya moto, yakishadondoka yanakuwa ya baridi, zamani watu wenye matatizo ya ngozi walikuwa wanakwenda kuoga, kunywa na kujipaka na wanapona lakini hakuna mtu anayelisemea hilo.

"Kama mto huo ungekuwa nje ya nchi, kama Swedeni ungeona kuna Watanzania wanakwenda na wanalipa fedha nyingi kuuangalia, tunatakiwa tupende vya kwetu," alihimiza.

Makatu alisema kuwa baada ya ziara hiyo itakayotumia siku 28, wanaamini watu walioko ndani na nje ya Tanzania wataelewa kwa undani vivutio vya utalii na desturi ya jamii ya Wahaya iliyoko Kagera.

Mkongwe huyo wa filamu alikumbusha kuwa zamani uchumi wa Kagera ulikuwa unategemea kahawa, lakini sasa kuna mabadiliko, kahawa si tegemeo tena.

Alisema kuwa hata chakula chao kikuu kilikuwa ndizi, lakini sasa utamaduni huo umewekwa kando, akisisitiza ipo haja ya kuurejesha kupitia matangazo.

Makatu alisema kilichokuwa kinakwamisha watalii kutoka nje ya nchi kumiminika kuingia mkoani Kagera, ni pamoja na kutokuwapo matangazo; watu wengi hawajui vivutio vilivyoko huko.

Alisema anaamini kuwa kutokana na umaarufu wa wasanii watakaofuatana nao katika ziara hiyo, dunia nzima itafahamu na watalii watamiminika kutembelea mkoani Kagera.

"Tunaimani baada ya ziara hiyo, watalii watamiminika sana. Serikali kuanzia uongozi wa mkoa, wote wanajua kuhusu sisi.

"Maombi yetu ni kupata nguvu kutoka taasisi mbalimbali ikiwamo serikali ili kuwafikisha wasanii huko kwa ajili ya kutangaza utalii. Watatumia zaidi ya siku 28 kutembelea na kuvitangaza vivutio hivyo," alisema.

Makatu alisema pamoja na kwamba wanahitaji nguvu ya wadau, tayari kuna baadhi wameanza kujitokeza japo hawatoshi kumudu gharama za kuwasafirisha wasanii 100 pamoja na waandishi wa habari.

"Tunaomba sana wadau wajitokeze kutuunga mkono ikiwamo serikali yenyewe, ili tupate fedha za kuendesha shughuli hiyo kuanzia usafiri, sehemu ya kulala wasanii na chakula kwa kipindi chote tutakachokuwa mkoani Kagera," Makatu aliwasilisha hoja yake kwa wadau.

Mkoa wa Kagera una vivutio vingi vya utalii ikiwa ni pamoja na mali kale, misitu ya asili na ya kupanda, uoto wa asili na fukwe za Ziwa Victoria.

# Mbunge aibua mapya utata kifo cha aliyechomwa visu 25

**Na Godfrey Mushi,** ROMBO

MBUNGE wa zamani wa Bunge la Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (EALA), Pamela Maasai, ameibua gumzo katika maziko ya Beatrice Minja (47), aliyekuwa mkazi wa Tarakea, Rombo, Mkoa wa Kilimanjaro baada ya kupoteza maisha katika shambulio la mauaji, baada ya kuchomwa visu 25 na mtu anayedaiwa kuwa mpenzi wake.

Mbunge huyo alidai familia nyingi katika Kijiji cha Mbomai, Tarakea, zimepoteza mke, waume, wazazi na watoto, kwa sababu ya uzembe wa watu kushindwa kuwajibika.

Kutokana na tishio la matukio ya ukatili katika wilaya hiyo, Pamela, ametuma ujumbe maalum kupitia maziko hayo, akimwomba Rais Samia Suluhu Hassan, Wilaya ya Rombo ipewe 'Special Intervention' (kuangaliwa kwa umakini) ili kuponya majeraha ya wananchi wake.

Alikuwa akitoa salaam za rambirambi baada ya ibada ya maziko ya Beatrice yaliyofanyika jana nyumbani kwao Kijiji cha Mbomai, Wilaya ya Rombo.

"Hilo si tukio la kwanza kutokea katika kijiji chetu cha Mbomai. Kumekuwa na mtiririko wa muda mrefu sana kwa matukio ya ajabu na ya kuogofya.

"Huu umati unaouona hapa ikifika saa 12 jioni, hakuna mtu anayetembea barabarani. Ni kwa sababu uhalifu katika maeneo haya umeongezeka kwa kiasi kikubwa, unyanyasaji umeongezeka kwa kiasi kikubwa, mauaji ya kikatili yameongezeka kwa kiasi kikubwa na yamkini kuna mahali ambapo wenye dhamana wangeweza kuchukua hatua tusingefika hapa.

...Watu wanalipa visasi, kwa namna ambayo watu wanafanya kwa sababu Jeshi la Polisi pamoja na serikali yetu labda imeshindwa kusimamia na kutenda haki.

"Wahalifu wanakamatwa wanaotenda mabaya, lakini baada ya muda mfupi unamkuta mtaani. Watu wanatenda matendo ya kinyama, lakini baada ya muda mfupi wanakuwa mtaani na kwa bahati mbaya sana wanakuja kudeal (kushughulika) na wale watu ambao walitoa ushirikiano.

"Tukio hili lilipata kificho kwa sababu raia wameshafika hatua ya kukata tamaa. Hawathubutu kusema, wanaogopa kwa sababu nitaonekanaje au nitakuja kuuawa.

"Hofu ni nyingi, lakini sisi kama watu ambao ni Wakristo, Waislam, pia tunapaswa kukumbuka imani yetu inatukumbusha suala la uwajibikaji.

"Ombi, ninaomba Mwakilishi wa Jeshi la Polisi anayetokea Dodoma, atusaidie kumfikisha salaam, naamini salaam hizi zitamfikia Mama Samia Suluhu Hassan, kwamba Wilaya ya Rombo inahitaji 'special intervention'.

Watu wanahitaji kupona majeraha, familia nyingi ni yatima. Familia nyingi watu wamepoteza mke, wamepoteza mume, watu wamepoteza wazazi, wamepoteza watoto kwa sababu ya uzembe wa watu kushindwa kuwajibika."

Beatrice, alipoteza maisha wakati akitetea uhai wake katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC iliyoko Moshi, Desemba 27, mwaka jana.

Kamishna Msaidizi wa Jeshi la Polisi kutoka Makao Makuu-Dodoma, ACP Ralph Meela alisema:

"Naomba tu niseme tukio hili lilitokea ni la kusikitisha sana na kwa utafiti ambao tumeona, wanaume ndio wanaleta shida sana. Matukio haya mengi wanaume ndio tunaongoza.

"Matukio mengine yanatokea kwa sababu ya tatizo la afya ya akili. Ifike mahali tuone kwamba sio kila uliye naye karibu ni salama sana.

"Kwa hiyo pale utakapoona kuna viashiria popote pale, utakapoona viashiria vyovyote vya mtu kutaka kutenda jambo baya, usije ukaishia kusema huyu ni mpenzi wangu, ni rafiki yangu ni mume wangu. Toa taarifa kwa watu wanaoweza kukusaidia na hasa Jeshi la Polisi."

Akihubiri katika ibada ya maziko ya Beatrice, Padri Timotheo Mwanda, Wakili wa Paroko, Parokia ya Mtakatifu Pius wa 10 wa Jimbo Katoliki la Moshi, alisema

Beatrice ameondoka akiwa nguzo kuu ya familia.

"Beatrice, ndiye tegemeo kuu la familia. Sijui watoto wake watafanyaje, lakini mama Sofina (mama yake Beatrice) ni mgonjwa, ni mzee na yuko hapa nyumbani.

"Katika kila jambo tafakari unalolifanya kwanza na ukumbuke mwisho wako ni nini, na ufanye kwa ukamilifu.

"Tunafanya mambo mengi, lakini haturidhiki na tunaingia tamaa. Kila mmoja wetu aridhike na wito wake.

...Tukio la leo la ukatili, mengi yanatendwa kwa asilimia 90 na watu wa karibu. Imani ulimwenguni imepungua, tena kwa watu walio wengi tu. Tunasikia matukio ya watu kuuawa na hawa wanaofanya hivi walilelewa katika misingi ya imani fulani fulani. Furaha yake si ya kudumu. Tunahangaikia mambo ya dunia zaidi."

Siku tatu baada ya Beatrice kufariki dunia wakati akipigania uhai wake katika Chumba cha Uangalizi Maalum (ICU), Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Kaskazini ya KCMC, mtuhumiwa wa shambulio hilo, Lucas Tarimo, naye alifariki dunia katika Hospitali Teule ya Huruma iliyoko Rombo.

Tarimo alifariki dunia Januari 2, mwaka huu majira ya saa 7:17 usiku akipatiwa matibabu, baada ya kunywa sumu ya kuua wadudu.

Novemba 12, alidaiwa kumshambulia Beatrice kwa kisu sehemu mbalimbali za mwili wake, alipofikishwa KCMC, alikaa ICU kwa siku 47.

Taarifa zinaeleza kuwa, familia ya Tarimo imepanga kufanya maziko yake Januari 5, mwaka huu, karibu na eneo la Mji wa Tarakea.

Kwa mujibu wa Msemaji wa Jeshi la Polisi, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP), David Misime, Tarimo, alimakatwa Desemba 31, 2023 majira ya alfajiri akiwa amejificha katika Kijiji cha Jema, Kata ya Oldonyosambu, Wilaya ya Ngorongoro, mkoani Arusha, akijiandaa kukimbilia nchi jirani.

# Kamati yaundwa kuchunguza kifo mjamzito

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

UONGOZI wilayani Kahama, mkoani Shinyanga umeunda timu maalum itakayochunguza kifo cha mjamzito Rachel William (19), aliyefariki dunia Desemba 28, mwaka jana kwa madai ya kukosa huduma katika Hospitali ya Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, akisubiri kujifungua.

Wakati timu ikiundwa kuchunguza suala hilo, taarifa kutoka Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kahama, zinabainisha kuwa watumishi wanaodaiwa kusababisha kifo cha mjamzito huyo, wameshasimamishwa kazi kupisha uchunguzi.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Kahama, Anderson Msumba, alibainisha kuundwa kwa timu hiyo jana wakati akijibu hoja mbalimbali katika kundi sogozi la WhatsApp la 'Kahama Politics' zilizohitaji kupata ufafanuzi juu ya hatua zilizochukuliwa kutokana na kifo hicho.

Alisema mjamzito huyo alipoteza maisha pamoja na kichanga tumboni kutokana na uzembe wa baadhi ya watoa huduma, hivyo aliomba radhi kwa niaba ya halmashauri kwa tukio hilo.

Msumba alisema tayari serikali imeshaunda timu ya kuchunguza tukio hilo, ikiundwa na Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita, ili kubaini chanzo.

"Mkuu wetu wa wilaya ameunda timu ya kuchunguza ya tukio hili na tunasubiri imalize kazi yake na tutatoa mrejesho wa hatua stahiki ambazo zitachukuliwa.

"Watumishi wanatakiwa kufanya kazi kwa weledi na kusimamia miiko na maadili ya kitaaluma ili kuhakikisha huduma zinazotolewa na serikali zinakuwa bora," alisema.

Alisisitiza kuwa wahusika wote waliokuwa zamu siku ya tukio hilo, wanajulikana na wameshatoa maelezo kwa maandishi kila mmoja na kwamba hawawezi kufanya mzaha kwenye maisha ya binadamu mwenzao na serikali ikakaa kimya, hivyo lazima wawajibishwe kisheria.

Msumba pia alisema jambo hilo wamelichukulia kwa umakini mkubwa na halikubaliki na hatua za awali zimeshachukuliwa, muda wowote Mstahiki Meya, Yahya Bundala, atatoa taarifa kwa umma ili kufahamu namna wanavyoendelea kuchukua hatua dhidi ya wahusika.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita, alisema alipokea taarifa hiyo kwa huzuni kubwa na hatua zinaendelea kuchukuliwa na ameunda timu mbili za kuchunguza tukio hilo.

Kwa mujibu wa mkuu wa wilaya, timu moja itachunguza matibabu na nyingine uongozi na zote ziko kazini zinaendelea na majukumu kama zilivyopangiwa.

Alisema serikali haiko tayari kuona wananchi wanapata matatizo kwenye maeneo ya kutolea huduma za afya, hasa kwa wajawazito, hivyo hawezi kufumbia macho suala hilo na hatua kali za kinidhamu kwa uzembe utakaobainika zitachukuliwa na sasa wamesimamishwa kazi kwa muda usiojulikana watumishi hao kupisha uchunguzi.

Rachel, mkazi wa Mtaa wa Mji Mwema katika Manispaa ya Kahama, alifariki dunia baada ya kudaiwa kunyimwa huduma ya kujifungua katika Hospitali ya Manispaa hiyo.

Ni tukio lililotokea Desemba 27, mwaka jana, saa nane usiku wakati mjamzito huyo alipofika hospitalini huko, lakini hakujifungua kwa wakati kwa madai ya kunyimwa huduma baada ya kuombwa rushwa na daktari aliyekuwa zamu.

# Mabadiliko Toto Afya yapeleka kilio kituo wenye uhitaji maalum

**Na Romana Mallya**

TAASISI ya Human Dreams Charity ya Kata ya Toangoma, wilayani Temeke Dar es Salaam, imesema kuwa baada ya serikali kuweka masharti mapya katika kadi ya Toto Afya ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), inatumia Sh. milioni tano kwa mwezi kutoa huduma za afya kwa watoto wenye mahitaji maalum inaowalea.

Huduma ambazo inatoa taasisi hiyo ni kusaidia watoto wenye ulemavu wa viungo wasio na wazazi kwa kupatiwa mahitaji yote muhimu kama vile chakula, malazi, matibabu, mavazi na mazoezi ya viungo.

Mwanzilishi wa taasisi hiyo, Nicole Mtawa, alibainisha hayo kikwazo hicho juzi wakati wa hafla ya chakula na watoto wenye mahitaji maalum katika kufunga mwaka 2023.

Hafla hiyo ilihudhuriwa na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, aliyejionea pia kazi inayofanywa na taasisi hiyo katika kuwapa huduma watoto hao na changamoto zake.

"Tunalea watoto 33 wasio na wazazi na watoto 15 wanaokuja katika kituo cha awali. Changamoto tulionayo; tangu serikali iweke masharti mapya katika kadi za Toto Afya, watoto yatima hawawezi kuunganishwa hasa kama shule haijatimiza watoto 100.

"Sasa hivi tunatumia gharama kubwa sana kupata matibabu kwa hawa watoto. Kwa makadirio ya matibabu kwa mwezi ni Sh. milioni tatu na dawa tunatumia takribani Sh. milioni mbili, jumla tunayotumia ni Sh. milioni tano," alisema.

Mtawa pia alisema wameanzisha kituo kingine cha Day Care Rehabilitation Center kwa ajili ya kuwafundisha na kuwapa mazoezi, hasa watoto wenye ulemavu wanaoishi katika mazingira magumu, kwa kuwachukua asubuhi na kuwarejesha kwao jioni.

Alisema lengo ni kuwawezesha wazazi au walezi wao kutumia muda ambao watoto watakuwa kituoni huko, kujishughulisha na biashara ndogo kwa ajili ya kujikumu.

Pia alisema changamoto nyingine wanayokabiliana nayo ni miundombinu ya barabara kuelekea katika taasisi hiyo ambayo huwapa ugumu pindi mtoto anapougua, hasa kipindi cha masika.

Kutokana na changamoto hiyo, Mtawa alikumbusha kumpoteza mtoto mmoja ambaye alikuwa anawahishwa hospitalini, lakini kikwazo kikawa miundombinu mibovu ya barabara.

Alisema wana madaktari wawili wa mazoezi ya viungo ambao ni wachache kulinganisha na idadi ya watoto na hawana nesi mwenye shahada katika taaluma hiyo.

Mtawa aliomba serikali kuwasaidia kupata madaktari wawili wa mazoezi ya viungo na nesi watakaowatembelea watoto na kuwapa huduma za afya angalau mara tatu kwa wiki kwa gharama za serikali.

Alitaja mahitaji mengine yanayohitajika katika taasisi hiyo ni vyakula na 'pampers' kutokana na bei na idadi ya watoto kuongezeka.

Kwa mujibu wa Mtawa, malengo ya taasisi ni watoto hao wapate nafuu na kuinuka ili kupelekwa shuleni kujiunga na wenzao kusoma. Alibainisha kuwa tayari kuna baadhi ya watoto wamefanikiwa.

Waziri Dorothy alipongeza taasisi hiyo kwa kazi kubwa inayofanya ya kutoa huduma kwa watoto hao kulingana na changamoto zao.

Kuhusu umuhimu wa kuwa na utaratibu rasmi wa jamii kusaidia wenye mahitaji maalum, Waziri Dorothy alisema ni wazo jema. Ameamua kuunda kamati ya kijamii itakayojadili, kuchambua na kuweka kwenye andiko wazo hilo.

"Mapendekezo mtayawasilisha wizarani ili na mimi niseme wazo hili ni jema, ili mwakani badala ya kutafuta watu kwa simu, tutawakuta wametangulia na misaada yao kwa wenye mahitaji maalum," alisema.

Kuhusu kuasili watoto, waziri huyo alisema ni changamoto ambayo wataifanyia kazi kwa kuangalia kuanzia Januari hadi Desemba mwaka jana, maombi yaliyopokewa yalikuwa mangapi, wangapi walipata watoto na wasiopata ni wangapi na sababu zake.

Akizungumzia bima ya afya ya watoto, Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Mohamed Mang'una, alisema wako katika mawasiliano na Wizara ya Afya ili kutafuta suluhu ya changamoto hiyo.

Kuhusu changamoto ya madaktari wa mazoezi ya viungo na nesi iliyotajwa na taasisi hiyo, Dk. Mang'una alisema wataangalia uwezekano wa wataalamu wachache walionao kwenda kituoni huko kutoa huduma.

Kuhusu 'pampers' zinazotumiwa na watoto hao, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, Elihuruma Mabelya, alisema amewasiliana na mdau ambaye atapeleka maboksi 150 huku akiahidi kutatua kero ya ubovu wa barabara.

Kwa mujibu wa Waziri Dorothy, Tanzania ina makao 342, vikiwa na watoto zaidi ya 12,000; vituo vya kulea watoto mchana ni 3,315.



Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Vifo hivi vya uzembe dhidi ya wajawazito visifumbiwe macho

**TAARIFA** za wajawazito kupoteza maisha wakati wa kujifungua zimekuwa zikiripotiwa mara kwa mara huku baadhi ya watuhumiwa kuchukuliwa hatua, zikiwamo kusimamishwa kazi au kuachishwa kazi kwa kukosa maadili kwa mujibu wa taratibu za mamlaka za uajiri.

Miongoni mwa sababu ambazo zimekuwa zikitolewa kwa wajawazito hao kupoteza maisha ama wenyewe au pamoja na watoto baada ya kujifungua ni kukosa huduma stahiki, lugha mbaya kutoka kwa wauguzi na wakunga au kuombwa rushwa na watoa huduma hao.

Katika tukio la hivi karibuni, ni katika Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga. Taarifa hizo zilisema mkazi wa Mtaa wa Mji Mwema katika Manispaa ya Kahama, Rachel William (19), amefariki dunia baada ya kudaiwa kunyimwa huduma ya kujifungua katika Hospitali ya Manispaa hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, tukio hilo lilitokea Desemba 27, mwaka jana, saa 8:00 usiku wakati mjamzito huyo alipofika hospitalini hapo lakini hakujifungua kwa wakati kwa madai ya kunyimwa huduma baada ya kuombwa rushwa na daktari aliyekuwa zamu. Pamoja na kumwona mjamzito huyo akitokwa na damu sehemu za siri, daktari huyo alishindwa kutumia ubinadamu na badala yake kumwomba rushwa ili toe huduma!

Jambo linaloonyesha kifo hicho kilisababishwa na uzembe au kukosa uwajibikaji, daktari anayetuhumiwa kufanya kitendo hicho alimpa mwanafamilia muhtasari kuhusu kifo cha Rachel ili atie saini achukue mwili wa mpendwa wake kwenda kuuzika bila kuandika jina lake. Hata alipofuatwa, daktari huyo alishindwa kutoa ushirikiano lakini waliuchukua mwili baada ya kushauriana na uongozi wa manispaa.

Hata hivyo, ni jambo la kutia moyo kwamba uongozi wa manispaa kupitia Mkurugenzi wake, Cleence Mkusa, umashindwa kuchukua hatua dhidi ya madaktari na wauguzi wa zamu wanaotuhumiwa kufanya uzembe na kusababisha kifo cha mjamzito huyo.

Suala la rushwa na uzembe katika sekta ya afya limekuwa sawa na donda ndugu kwa muda mrefu na limesababisha wagonjwa wengi wakiwamo wajawazito, kupoteza maisha. Pamoja na hatua kuchukuliwa dhidi ya baadhi ya wahusika, bado tatizo hilo linazidi kuota mizizi.

Chanzo kikubwa ni baadhi ya madaktari na wauguzi wasio na maadili kuendeleza rushwa kabla ya kutoa huduma. Mbali na kifo cha mjamzito huyo, Mbunge wa Usheru, Emmanuel Cherehani, alitoa mfano wa kifo cha mama aliyepoteza kichanga baada ya kushindwa kutoa rushwa ya Sh. 150,000 aliyoombwa na watoa huduma katika Kituo cha Afya cha Ukune.

Mifano hiyo miwili iliyojulikana ni katika wilaya moja tu ya Kahama. Je, nchini kote hali ikoje? Matukio yanaripotiwa na hatua stahiki kuchukuliwa au watu wanalindana kwa sababu wengi wako katika mkumbo huo?

Ni dhahiri kwamba matukio ya namna hiyo yameenea sehemu mbalimbali nchini lakini hatua kwa kiasi kikubwa zimekuwa hazichukuliwi dhidi ya wanaotuhumiwa kufanya vitendo hivyo na kuharibu taswira ya fani ya tiba na uuguzi.

Katika hospitali moja kubwa jijini Dar es Salaam, mjamzito mmoja nusura apoteze maisha baada ya kukaa siku nne mtoto akiwa amefia tumboni. Wakati wanafamilia wakifuatilia baada ya kufikishwa katika hospitali hiyo kwa rufani kutoka ngazi za chini, madaktari na manesi waliokuwa wakimhudumia walikuwa wakitoa lugha zisizo na staha zikiwamo 'usitufundishe kazi tunajua tunachofanya'.

Ni wakati mwafaka sasa mamlaka zinazohusika na afya zikaamka kutoka usingizini kutokana na kuota mizizi kwa taarifa kama hizo ambazo zinasababisha vifo vya wajawazito na watoto. Kamwe matukio kama hayo yasifumbiwe macho kwani mzaha mzaha hutumbuka usaha.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com



## Muungwana Lazima Nilonge



Sabato Kasika

# LATRA malizeni sintofahamu hii ya nauli za daladala Dar

**NAULI** mpya ya daladala na mabasi yanayoenda mikoani, zilianza kutumika Desemba 8, mwaka jana.

Tangu wakati huo kumekuwapo na sintofahamu inayosababisha usumbufu kwa abiria.

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Ardhini (LATRA), ilitangaza ongezeko la nauli mpya, baada ya kutokuwapo kile ambacho mamlaka hiyo ilieleza kuwa ni pingamizi kutoka kwa wadau wa usafirishaji.

Wakati huu ambao nauli imeongezeka, kumekuwapo utata katika utozaji nauli hizo, hasa kwenye daladala, huku ikielezwa kuwa baadhi ya makondakta wanatoza bila kuzingatia umbali.

Mfano mmojawapo unatajwa ni nauli ya daladala kutoka Mbezi Mwisho hadi Mwenge Dar es Salaam haieleweki, kwani baadhi ya makondakta wanatoza shilingi 800 na wengine 700.

Katika mazingira hayo, inakuwa vigumu kuelewa kuwa nauli halali ni ipi, ingependeza kama LATRA itabandika chati inayoonyesha nauli halisi ndani ya daladala, ili kusiwapo msuguano kati ya abiria na makondakta.

Utozaji nauli ulivyo sasa, ni vigumu abiria kujua kiwango cha nauli kilichowekwa na LATRA. Kutozwa nauli kwa viwango tofauti katika 'ruti' moja, ni sawa na kumwongozea abiria gharama za maisha.

Orodha ya nauli elekezi ikibandikwa ndani ya daladala, inasaidia kupunguza malalamiko ambayo wakati mwingine mwisho wake huwa ni hauwezekani, LATRA watoe elimu itakayowezesha abiria na makonda kutimiza wajibu wao inavyotakiwa, kwani katika mazingira ya ugumu wa maisha hakuna anayekubali kuchukuliwa fedha kirahisi.

Ikumbukwe kuwa nauli za daladala na mabasi zimepanda, madereva wa bajaj nao wamepandisha. Umbali ambao daladala ilikuwa inatoza nauli ya shilingi 500, wao sasa wanatoza shilingi 700.

Yaani ni kama abiria wanapigwa huku na kule, kitendo ambacho katika mazingira ya maisha ya sasa unakuwa mzigo, hasa pale ambapo wakati wa jioni inapandishwa zaidi ya ile iliopangwa na LATRA.

**Tangu wakati huo kumekuwapo na sintofahamu inayosababisha usumbufu kwa abiria.**

Kwa madereva na makondakta wa daladala, ni jambo la kawaida kwao kuongeza nauli kutoka shilingi 600 hadi hadi 1000, hasa wakati wa jioni hadi usiku, kitendo hicho ni sawa na kuwaongezea gharama ya maisha.

Ingependeza kama mamlaka husika inapopandisha nauli na kufanya ufuatiliaji kama inatumika kulingana na jinsi ilivyopanga, kwani ninadhani kutofuatilia ndiko kunakosababisha usumbufu huo.

Wakati mwingine mtu anaweza kutoka kwenye mihangaiko au anakwenda kwenye mihangaiko akiwa na nauli ambayo imepangwa na LATRA, lakini anaambiwa haitoshi, kwa kuwa tu wameongeza yao.

Lakini kama LATRA wakifanya ufuatiliaji, ninadhani wanaweza kugundua kero nyingi ambazo abiria wanakutana nazo, hasa utozaji wa nauli usiozingatia nauli elekezi zilizopangwa na mamlaka hiyo.

Inaumiza kuona abiria wanalipa viwango vya nauli ambavyo havijaidhinishwa na LATRA, huku baadhi ya abiria wanaoshabikia nauli za juu na kusababisha maumivu kwa wenzao.

Kama nilivyoeleza, mbali na mkanganyiko wa viwango vya nauli tofauti zinazotozwa kwa ruti ya Mbezi Mwisho hadi Mwenge, kuna upandishaji wa nauli kuanzia jioni hadi usiku, kinyume na ile inayotakiwa kutozwa.

Ninaamini kwamba, iwapo mamlaka husika itafuatilia mkanganyiko huo, itasaidia kuwaondolea wananchi usumbufu wanaokutana nao wakati wa usiku wanaporudi kutoka kwenye mihangaiko ya kila siku.

Lakini, abiria nao wangekuwa na uthubutu kutoa taarifa kwenye vyombo husika badala ya kuendelea kuumia huku madereva na makondakta wakipata jeuri kwa kuamini hakuna wa kuwachukulia hatua za kisheria.

HABARI KITAIFA

# Biteko akoleza moto maoni miswada sheria ya uchaguzi, vyama vya siasa

**Na Mwandishi Wetu,**
GEITA

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, amewahimiza Watanzania kushiriki kutoa maoni kuhusu muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa mwaka 2023.

Miswada mingine ambayo iliwasilishwa bungeni Novemba, mwaka jana, na wananchi kutakiwa kutoa maoni ni wa Sheria ya Tume ya Uchaguzi wa mwaka 2023 na wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa wa mwaka 2023.

Kwa kufanya hivyo, Biteko amesema ni sehemu ya kuunga mkono jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan za kujenga Tanzania iliyo bora zaidi katika nyanja zote za kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Dk. Biteko amesema hayo juzi wakati akizungumza na wananchi wa Wilaya ya Mbogwe mkoani hapa katika sherehe za kuaga mwaka 2023 na kuukaribisha mwaka 2024 zilizoandaliwa na Mbunge wa Mbogwe, Nicodemus Maganga, na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali mkoani Geita wakiongozwa na Mkuu wa Mkoa, Martine Shigella.

"Rais amepeleka miswada hii bungeni iliyosomwa wakati wa Mkutano wa 13 wa Bunge na tangazo limeshatoka la kuwaomba wananchi kwenda kutoa maoni yao bungeni kuanzia Januari 6 hadi 10, 2024 kuhusu marekebisho ya sheria hizi. Niwaombe Watanzania nendeni mkatoe maoni yenu ili kujenga Tanzania iliyo bora kuliko kubaki nyuma kulalamika," alisisitiza.

Dk. Biteko alisema Rais Samia anafanya kazi kubwa ya kuwaunganisha Watanzania wa vyama, dini na makabila mbalimbali na anasikiliza malalamiko ya makundi mbalimbali na kuyafanyia kazi. Alitoa mfano wa suala la kuruhusu vyama vya siasa kufanya mikutano ya hadhara ili kueleza sera zao na kwamba nia ya Rais ni kujenga mshikamano na umoja nchini.

Kuhusu uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika baadaye mwaka huu, Dk. Biteko aliwahimiza wananchi kuchagua viongozi bora na kwamba watu wasigawanyike na kufarakana kwa sababu ya uchaguzi bali waungane kwa kuzungumza yanayowaunganisha kama vile barabara, maji, umeme na wasiruhusu mtu kupandikiza chuki kati yao.

Katika salamu zake za Mwaka Mpya, Biteko aliwasisitiza Watanzania kupendana, kuthaminiana, kuvumiliana, kusameheana, kuwa na shukrani, kusaidiana na kumfanya mtu mwingine afurahi, lengo likiwa ni kujiletea maendeleo.

Kuhusu hali ya upatikanaji umeme wilayani Mbogwe, Dk. Biteko alisema itaendelea kuimarika kwa kuwa imejengwa njia mpya ambayo itapeleka umeme wilayani humo kutokea kituo cha Nyakanazi. Pia alisema itajengwa njia nyingine ambayo itapeleka umeme Mbogwe kutokea Kahama pamoja na kituo cha kupoza na kusambaza umeme wilayani humo.

Awali, akiwasilisha salamu za Mwaka Mpya, Shigella alisema anaridhishwa na utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwenye Wilaya ya Mbogwe ikiwamo elimu, maji, umeme, barabara na afya.

Kuhusu utekelezaji wa miradi ya umeme mkoani Geita, Shigella alisema asilimia 90 ya vijiji vya mkoa huo tayari vimeshapatiwa umeme na vijiji 50 vilivyosalia kazi za kusambaza zinaendelea ikijumuisha mipango ya kupeleka umeme hadi kwenye vitongoji.

Naye Mbunge wa Mbogwe, Maganga, alimshukuru Naibu Waziri Mkuu kwa kufika Mbogwe kushiriki na wananchi katika sherehe hizo na kuongeza kuwa Mbogwe imejipanga kutekeleza miradi ya maendeleo ikiwamo sekta ya madini kuendelea kufanya vizuri.



Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Siti Abbas Ali (kushoto), akizungumza na viongozi wa dini eneo la Sebulani, Wilaya ya Mjini jana na kuwahimiza kutumia nafasi yao kuelimisha jamii kuepuka vitendo viovu na kusimamia maadili mema. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kinana: Hakuna dhambi kiongozi anapomaliza muda kupewa tena

**Na Mwandishi Wetu,**
RUANGWA

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tanzania Bara, Abdulrahman Kinana, amesema hakuna dhambi kwa kiongozi aliyeko madarakani anapomaliza awamu ya kwanza kupewa awamu ya pili ili aendelee kuongoza.

Kauli ya Kinana inatokana na ombi la Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, Mbunge wa Ruangwa kuishauri Kamati Kuu na Halmashauri Kuu ya CCM iridhie kutoa fomu moja ya urais katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 na fomu hiyo ni ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Akizungumza mbele ya wajumbe wa Mkutano Mkuu Maalumu wa CCM Wilaya ya Ruangwa mkoani Lindi, kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM, Kinana alisema kila aliyesimama amezungumza mambo mazuri yanayofanywa na Rais Dk. Samia ya kuleta maendeleo ya wananchi.

"Waziri Mkuu pamoja na wote mliosimama mmezungumzia kazi nzuri inayofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita. Mambo yanayofanyika katika nchi hii ni makubwa sana na katika kila eneo, fedha ambazo zimekwenda katika halmashauri ni nyingi.

"Madarasa yanajengwa bila ya watu kuchangishwa, vituo vya afya vinajengwa, barabara zinajengwa. Nilikuwa Waziri wa Ulinzi nimezunguka kote huku ikiwamo Ruangwa, hakukua na barabara za lami. Vile vile, alisema Rais Samia anaonesha njia kwa kupanga, kutafuta mikakati na kuweka vipaumbele na sasa Watanzania wanajivunia mafanikio na wana-CCM wanaposema mgombea waliyenaye anatosha 2025 wanasababu kwa kutambua mchango wake katika taifa.

Alisema, utamaduni wa CCM ni kumwacha Rais aliyepo madarakani anapomaliza awamu ya kwanza kupewa nafasi kwa awamu ya pili, imefanyika hivyo kwa Rais mstaafu Ali Hassan Mwinyi, Benjamin Mkapa, Jakaya Kikwete na Dk. John Magufuli ambaye alifariki dunia akiendelea na uongozi kwa muhula wa pili.

"Wana Ruangwa mmeleta mageuzi makubwa, nilipata nafasi ya kupita hapa miaka ya mwaka 1980, 1990 na 2000, kuna maendeleo makubwa yamefanyika. Msingi wa kwanza wa maendeleo ni watu kuwa wamoja," alisema.

Kinana alisema kuwa Waziri Mkuu ni mpole, mcheshi na hizo ndizo sifa kiongozi anatakiwa kuwa nazo huku akieleza wananchi wamempa sifa nyingi kiasi cha kueleza wanataka mbunge wao aendelee katika miaka yote na hakuna wa kumpinga.

Alisema anahakikka wananchi wakiendelea kumpa nafasi Majaliwa kuwa mbunge wao ili wilaya hiyo iwe na mabadiliko makubwa kuliko wilaya nyingine.

"Bahati nzuri nina uwezo wa kujua tofauti, lakini hapa kwenu hakuna, wote mko kitu kimoja, watu wa Ruangwa hawapotezi muda kuzungumzia watu, wanapoteza muda kuzungumzia maendeleo."

Awali, Waziri Mkuu wakati anaelezea utekelezaji wa ilani aliomba Kamati Kuu na Halmashauri Kuu watoe fomu moja ya Dk. Samia Suluhu Hassan mwaka 2025 kama mgombea pekee urais kupitia CCM.

"Tukiwa na uhakika haya yanayofanyika leo, maajabu ambayo tunayaona yataendelea na sisi wana Ruangwa tunanufaika. Wilaya ya Ruangwa ni changa, lakini kwa kushirikiana na Rais Dk. Samia maendeleo yamepatikana na leo tunaweza kuringa kwa hatua nzuri iliyofikiwa na huduma za maendeleo ambazo zinatolewa," alisema.

Alisema Wilaya ya Ruangwa ni mpya inachangamoto nyingi, lakini kwa ushirikiano wa pamoja wa Dk. Samia Suluhu Hassan wameendelea kuratibu mahitaji na matakwa ya wananchi katika kuhudumia jamii.

KABWELA FADHILI MOHAMED



# Majaliwa asema Samia kielelezo mafanikio

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema Rais Samia Suluhu Hassan amekuwa kielelezo cha mafanikio makubwa yanayofikiwa nchini, hivyo kuliwezesha taifa kuendelea kupata utulivu, maelewano na kasi kubwa ya maendeleo kupitia maono, maelekezo na mipango mbalimbali.

Majaliwa ambaye ni Mbunge wa Ruangwa mkoani Lindi, aliyasema hayo juzi kwenye Mkutano Mkuu Maalumu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Ruangwa uliofanyika katika Uwanja wa Likangara, Ruangwa.

"Sisi wana-Ruangwa tunatoa shukurani za dhati kwa Mheshimiwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kuridhia na kuwezesha utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo hapa wilayani na kitaifa.

Kwa hakika Mheshimiwa Rais amekuwa kielelezo cha misingi ya uongozi na utawala bora, hivyo sisi Wana - CCM tunaendelea kutembea kifua mbele na tunamhakikishia kuwa mazingira aliyoyaweka yatatuwezesha kushinda uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka huu na Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025," alisema.

Aliyataja baadhi ya masuala makubwa ya kitaifa yaliyofanywa na Rais Samia tangu alipoingia madarakani ni pamoja na kuendeleza miradi ya kimkakati ukiwamo ujenzi wa Bwawa la Kuzalisha Umeme la Mwalimu Nyerere, ujenzi wa Reli ya Kisasa na madaraja makubwa likiwamo la Kigongo - Busisi.

Kwa mujibu wa Majaliwa, lengo la miradi hiyo ni ili kukuza uchumi, kuongeza fursa za ajira na kufikia malengo yaliyokusudiwa katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM.

Waziri Mkuu alisema mafanikio mengine ni kurejesha taswira ya Tanzania katika medani za kimataifa na kuimarisha diplomasia ya uchumi. "Kwa kufanya hivi Mheshimiwa Rais amefungua fursa mbalimbali ukiwamo uwekezaji, mitaji, masoko ya bidhaa, ongezeko la watalii, kubidhaisha lugha ya Kiswahili na utatuzi wa changamoto za kibiashara na nchi jirani," alisema.

Pia alisema Rais ameiwezesha nchi kuwa na mtangamano wa kisiasa unaojumuisha siasa safi, za kistaarabu na zinazoheshimu mawazo ya kila mtu, hatua ambayo imefanya hali ya siasa nchini kuwa tulivu chini ya sera ya 4R (Reconciliation, Resilience, Reform and Rebuilding), kwa Kiswahili ni Maridhiano, Ustahimilivu, Mageuzi na Ujenzi wa Taifa.

Waziri Mkuu Majaliwa ametaja baadhi ya mafanikio yaliyopatikana wilayani Ruangwa tangu serikali ya awamu ya sita ilipoingia madarakani ni pamoja na uboreshwaji wa huduma mbalimbali za kijamii zikiwamo za afya, elimu, maji, miundombinu ya barabara na kilimo na hivyo kuwawezesha wananchi kupata maendeleo.

Kuhusu huduma za afya, Majaliwa alisema serikali imewezesha ujenzi wa hospitali ya wilaya; ujenzi wa vituo vya afya vipya vinne katika kata za Malolo, Nangurugai, Narungombe na Namichiga; ujenzi wa zahanati mpya tisa za Namungo, Mbangara, Muhuru, Namkatila, Mkaranga, Mihewe, Lipande, Mkutingome na Mtakuja, hivyo kuwawezesha wananchi kupata huduma karibu na makazi yao na kwa wakati.



Mafundi wakiendelea na ujenzi wa daraja la chini la treni katika eneo la Kamata jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Wakumbushwa kukemea mmomonyoko wa maadili

**Na Sabato Kasika**

MKURUGENZI wa Idara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Siti Abbas Ali, amewakumbusha viongozi wa dini kutumia nafasi yao kuelimisha jamii kuachana na vitendo viovu ili nchi iwe salama.

Siti aliyasema hayo jana alipokuwa akifungua kikao kazi cha viongozi hao kilichofanyika Sebleni Wilaya ya Mjini na kukumbusha umuhimu wao katika kuepusha mmomonyoko wa maadili.

"Lengo la kukutana nanyi ni kutaka kubadilishana mawazo na kuweka mikakati itakayomaliza vitendo viovu vinavyochangiwa na mmomonyoko wa maadili ndani ya jamii," alisema Siti.

Mkurugenzi huyo alisema idara yake itajitahidi kukutana na viongozi hao mara kwa mara ili kukumbushana na kutekeleza kwa ufanisi majukumu mbalimbali walioojipangia.

Mwenyekiti wa viongozi wa dini wa harakati hizo, Mwazini Jogoo, aliahidi kushirikiana na Idara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ili kufikia malengo ya serikali ya kupambana na vitendo vya udhalilishaji.

"Tumekuwa tukitoa elimu dhidi ya vitendo vya udhalilishaji katika maeneo mbalimbali ikiwamo madrasa, misikiti na kanisani, lakini tunakutana na ugumu kwenye baadhi ya maeneo," alisema Jogoo.

Mwenyekiti huyo alisema kuna haja kwa idara hiyo kukaa na wale wanaoweka ugumu, ili viongozi hao waweze kufanya kazi ya kutoa elimu kwa ufanisi.

"Lakini kuna changamoto ya mahudhurio hafifu ya wananchi katika mikutano pia tunakabiliwa na tatizo la ukosefu wa fedha za kuendeshea miradi tulioanzisha katika shehia mbalimbali," alisema.

# Alliance One yawapa msaada waathirika maporomoko Hanang'

**Na Mwandishi Wetu,** HANANG'

KAMPUNI ya Tumbaku ya Alliance One yenye makao yake makuu mkoani Morogoro, imekabidhi msaada wa bidhaa mbalimbali kwa waathirika wa maporomoko ya tope, magogo na mawe huko Katesh, wilayani Hanang, bidhaa hizo zikiwa na thamani ya Sh. milioni 25.

Msemaji wa kampuni hiyo, Wakili John Magoti, alisema juzi kuwa kampuni imepokea kwa majonzi taarifa za janga hilo, hivyo inampa pole Rais Samia Suluhu Hassan kwa kupoteza Watanzania kutokana na janga hilo.

"Kampuni ya Alliance One kama kupitia sera yake ya uwajibikaji kwa jamii, Mkurugenzi Mkuu pamoja na menejimenti yote tumefikiria na kufikia uamuzi kuwa tutoe misaada mbalimbali ikiwamo lishe ya watoto wadogo (baby formula), mavazi kwa ajili ya familia zote kwa maana ya watu wazima na wadogo," alisema.

Aliongeza kuwa katika kuwasitiri waathirika hao ambao wamepoteza vitu vyao, wamepeleka mablanketi.

Akipokea msaada huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hanang, Francis Namaungo, alishukuru kampuni hiyo, akisema wananchi wa Hanang' wanapokea misaada hiyo kwa moyo mkunjufu.

"Misaada huu kwa waathirika hawa wa maporomoko ya matope, magogo, mawe na taka zingine kwa walengwa hawa umekuja kwa wakati mwafaka," alisema.

Alisema, "hii lishe mlioleta kwa ajili ya watoto ambao ni taifa la kesho ni muhimu. Kwa kupatiwa lishe bora, watoto wadogo hawa watakuja kumudu vyema majukumu yao kwa taifa lao ukubwani.

"Lakini pia kwa mavazi haya, yatawasaidia sana, kwani wengi wao waliondokewa kabisa na mavazi, chakula, mali zao wakati wa janga hili. Hivyo, hili linagusa msaada mkubwa katika maisha yao.

"Kwa niaba ya Wanahanang wote, ninasema asante, ninachowahakikishia tu ni kwamba msaada huu utawafikia walengwa wanaostahili kadri ambavyo utaratibu wa kiserikali kwa idadi ya waliopata maafa na idadi ya misaada uliotolewa watapewa kwa uwiano unaotakiwa.

"Karibuni tena, waambieni na wengine kwamba tunahitaji na vifaa vya ujenzi, kwa sababu wapo pia waliopoteza makazi, hivyo tunafanya utaratibu wa kuangalia kuwarejesha katika makazi mengine kwa kuwajengea, hivyo mahitaji ya ujenzi huo yanahitajika pia."

Mmoja wa waathirika wa janga hilo waliohifadhiwa kwenye Shule ya Sekondari ya Katesh, Zepetu Murda alisema hakutoka na kitu chochote mkononi siku ya janga hilo, zaidi ya uhai wake.

"Kwa mfano, mimi nilitoka kwenye nyumba yangu nikiwa uchi wa mnyama. Wasamalia wema walipokuwa wananiokoa ndipo walinifunika kwa mavazi yao na kunisitiri nguo hizi na zingine ninazoendelea kupewa na wasamalia wema," alisema na kuongeza kuwa anategemea sana msaada wa serikali na wasamalia wema kwa sasa.

Mwathirika mwingine, Stephano Robert ambaye naye miongoni mwa kundi la mwisho la waathirika waliosalia shuleni huko, alisema tukio hilo lilitokea kwa namna ya kushtukiza, saa 12:15 asubuhi.

Alisema walichofanya ni kutafuta namna ya haraka kujiokoa kwa kukimbilia kwa majirani kwa kuwa nyumba zao tayari zilikuwa zinazidi kujaa tope huku likiongezeka. Wakati wa mbio hizo vyombo vyao walivitelekeza na hawana kitu walichosalia nacho.

Kampuni ya Alliance One katika mpango wake wa huduma kwa jamii inatenga Sh. milioni 400 kila mwaka kwa ajili ya kusaidia jamii katika maeneo ya maji, elimu na afya.

Ilifungua kiwanda chake cha usindikaji mnamo 1998 na imekuwa inafanya kazi kwa mafanikio tangu wakati huo bila kukosa msimu wowote wa mazao na kwa sasa ina wafanyakazi 350 wa kudumu na wanaolipwa pensheni pamoja na wafanyakazi wa msimu 3,000 kila mwaka.

## Maji bwerere Simanjiro na Kiteto

**Na Jaliwason Jasson,**
MANYARA

HATIMAYE wakazi 7,500 wa Wilaya ya Simanjiro na Kiteto mkoani Manyara wameondokana na kero ya muda mrefu ya kusaka maji baada ya kukamilika kwa Mradi wa Maji wa Magungu/Nati.

Wakazi hao wa vijiji vya Magungu na Nati, wanawake na watoto, walikuwa wakipoteza muda mwingi usiku kucha na mchana kutwa kwenda kusaka maji kata jirani na kushindwa kufanya shughuli za kiuchumi.

Akizungumzia mradi huo jana, Kaimu Meneja wa Wakala wa Maji Vijijini wa Wilaya ya Simanjiro (RUWASA), Boniface Mushi, alisema makali ya mgawo wa maji na wakati mwingine kukosa, umepungua baada ya upatikanaji wa maji hayo kwa sasa kufikia asilimia 66.

Alisema wakazi 2,174 kwa Kijiji cha Magungu, ndio wanaohudumiwa na mradi huo sawa na asilimia 22.

Akizungumzia hali ya upatikanaji wa maji kwa wananchi wake, Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Magungu, Christopher Kidao, alisema mradi huo umekidhi mahitaji yao wote.

Wakazi wa Magungu walikuwa wanapata maji umbali wa kilometa moja tofauti na sera ya maji inataka mwananchi apate huduma hiyo umbali wa mita 400.

Meneja wa RUWASA wa Wilaya ya Kiteto, Stephano Mbarouk, alisema mradi huo unaohudumia vijiji viwili kwa vilula vya kuchotea maji 15 na kituo kimoja cha kunyweshea mifugo.

Mradi huo wa Magugu/Nati, umeigharimu Serikali zaidi ya Shilingi bilioni 1.3 hadi kukamilika kwake.

Mkazi wa Magungu, Matita Kwandi alisema walikuwa wanakesha kutafuta maji na kwamba kwa sasa wameondokana na adha hiyo baada ya serikali kuwapelekea huduma hiyo.

"Kwa sasa kila mahali kuna maji mpaka kwenye vitongoji tunaishukru sana serikali kwa kutuletea maji," alisema Kwandi

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Simanjiro, Moza Mlutu alisema kwa sasa maji wanapata wakati wote.

Mkazi wa Kiteto, Lonad Kulingi alisema wanaishukru serikali kwa kuwapelekea maji karibu na makazi yao na kuwaondolea adha hiyo na kunusuru mifugo yao kufa kwa ukame.

**Meneja wa RUWASA wa Wilaya ya Kiteto, Stephano Mbarouk, alisema mradi huo unaohudumia vijiji viwili kwa vilula vya kuchotea maji 15 na kituo kimoja cha kunyweshea mifugo.**

# Uhaba wa sukari waikumba mikoa ya Kanda Kaskazini

**Na Jaliwason Jasson,**
BABATI

SERIKALI imesema uhaba wa sukari ulioikumba mikoa ya Kanda ya Kaskazini ya Kilimanjaro, Arusha, Manyara na Tanga unatokana na Kiwanda cha Sukari cha TPC na Manyara Sugar kusitisha uzalishaji kwa kukosa malighafi.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji wakati akitoa ufafanuzi kutokana na adha ya ukosefu wa bidhaa hiyo inayowakumba wakazi wa mikoa hiyo baada ya kutembelea Kiwanda cha Sukari cha Manyara Sugar kilichopo Kijiji cha Matufa Wilaya ya Babati mkoani Manyara.

Dk. Kijaji alisema ili kukabiliana na uhaba huo, serikali inaangalia utaratibu wa kusambaza kutoka mikoa yenye sukari nyingi kwenda kwa yenye upungufu ili kudhibiti mfumuko wa bei kwa bidhaa hiyo.

Wakati Waziri Kijaji akitafuta ufumbuzi wa kukabiliana na tatizo hilo, kilo moja ya sukari kwa sasa inauzwa Shilingi 3,200 kwa bei ya rejareja katika Mji wa Babati na kwa Karatu kuanzia Sh. 3,800 hadi Sh.4,000.

Akizungumzia uamuzi wa Manyara Sugar kusitisha uzalishaji, Ofisa Uhusiano wa Kiwanda hicho, John Jeu, alisema ni kutokana na ukosefu wa malighafi.

"Tunawaomba viongozi ngazi zote kuhamasisha kilimo cha miwa kwa wananchi ili kuondoa shida ya ukosefu wa sukari na bei kupanda," alisema na kuongeza kuwa: "Tunashauri kuwapo kwa mpango wa muda mrefu wa uchimbaji wa mabwawa makubwa yatakayosaidia kuhifadhi maji kwa ajili ya umwagiliaji ili kuwaondolea wakulima wa miwa utegemezi wa msimu wa mvua pekee."

Ili kumaliza tatizo la malighafi hasa miwa, serikali inapaswa kuandaa mpango wa muda mrefu wa kuwa na visima zaidi ya 680 kati ya hivyo, 150 vitachimbwa Wilaya ya Babati na 30 kwenye mashamba ya miwa ya Magugu.

Alipoulizwa kuhusu upatikanaji wa sukari inayouzwa kwa sasa, mfanyabiashara, Peter Mallya wa mjini Babati, alisema wanapata kwa tabu baada ya Kiwanda cha TPC walilokuwa wanachua kupunguza uzalishaji.




Mjumbe wa Kamati ya Siasa ya CCM Wilaya ya Simanjiro, Mkoani Manyara, Oloisolo Materi (katikati), akiwaongoza wanachama wa Jumuiya ya Vijana wa CCM kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo ya elimu, afya na maji kwenye Kata ya Terrat juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Kiama mtandao wezi wa mifugo chaja

**Na Godfrey Mushi,**
NGORONGORO

KIKOSI Maalum cha Kuzuia Wizi wa Mifugo Nchini (STPU) cha Jeshi la Polisi kimetangaza kiama dhidi ya wezi wa mifugo nchini ili kutokomeza vitendo hivyo.

Kwa mujibu wa Kamanda wa STPU nchini, Simon Pasua hatua hiyo imekuja baada ya kupata orodha ndefu ya watuhumiwa hao na wanaopanga njama za kutekeleza wizi huo.

Kwa mujibu wa Kamanda Pasua, kwa sasa kikosi hicho kinachunguza na kufuatilia mienendo ya watuhumiwa hao wanaowavuruga wafugaji na kuwaachia machungu baada ya kutekeleza uhalifu wao. Kamanda huyo, alitangaza mpango wao huo wakati akizungumza na wananchi waliokubali kuhama kwa hiyari kutoka eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) kwenda Kijiji cha Msomera Wilaya ya Handeni mkoani Tanga kupisha shughuli za uhifadhi.

"Naonya na natoa tahadhari achaneni na mipango hiyo. Jamii ya kifugaji inapaswa kutembea kifua mbele kwa sababu kikosi hiki kitahakikisha mifugo inakuwa salama," alionya na kuongeza kuwa:

"Tayari Jeshi la Polisi kupitia STPU limeweka utaratibu mzuri na Polisi Kata ambao wameshaunda vikundi vya ulinzi wa mifugo yenu. STPU kimepokea majina ya baadhi ya watu wanaojihusisha na wizi wa mifugo."

Kwa upande mwingine, Pasua aliiomba jamii ya wafugaji wa Kimasai kuendelea kushirikiana na Polisi hasa kikosi hicho kwa kutoa taarifa za baadhi ya watuhumiwa ili wachukuliwe hatua.





# JWTZ lawaomba wananchi waliovamia maeneo kuondoka

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MKUU wa Kamandi ya Anga kutoka Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ), Meja Jenerali Shaaban Mani, ameiomba serikali mkoani hapa kulipatia jeshi hilo maeneo yaliyovamiwa na wananchi ili waweze kufanya shughuli zao kwa ufanisi zaidi.

Alitoa ombi hilo juzi alipofanya mazungumzo na Katibu Tawala wa Mkoa wa Mwanza, Balandya Elikana na kusema maeneo ya jeshi ni lazima yawe mbali na makazi ya wananchi ili kutokuingiliwa katika shughuli zao.

"Kitendo cha nyumba za raia kuwa karibu yetu ni hatari pia kwa usalama wa nchi kwa mtu atakaye kuwa na nia mbaya, alisema Meja Jenerali Mani.


Katika hatua nyingine Meja Jenerali Mani alisema jeshi hilo lipo tayari kuhusishwa kikamilifu katika ulinzi wa miradi inayotekelezwa na serikali kutokana na teknolojia inavyozidi kushika kasi, hivyo kama msaada utahitajika ni vyema jeshi hilo lipewe taarifa ili lijipange vizuri katika kutekeleza majukumu hayo.

"Sisi kama jeshi ni wajibu wetu kuhakikisha muda wote taifa lipo salama, nimefika Mwanza ili kukagua miundombinu yetu iliyopo chini ya kikosi cha anga na kama kuna changamoto inapaswa kuzifanyia kazi haraka," alisema Meja Jenerali Mani. Katibu Tawala wa Mkoa wa Mwanza, Balandya Elikana, aliahidi kushirikiana na jeshi hilo kwenye miradi mbalimbali ya kimkakati iliyopo mkoani hapa ili iimalike kiulinzi na kiusalama kwa tija ya wananchi.

"Tuliona mwaka 1978 wakati wa vita dhidi ya Idd Amin Daraja la Mto Kagera lilivyo shambuliwa na adui hilo ni somo kwetu vikosi vya jeshi kuwa karibu na miundombinu kama hiyo," alifafanua Elikana.

Aidha, alisema Mkoa wa Mwanza una miradi mingi inayoendelea kujengewa kuanzia Reli ya Kisasa, Daraja la Magufuli na meli ya abiria ya Mv Mwanza na Kituo cha Kimataifa cha Ulinzi na Uokoaji Ziwa Victoria kinachotarajiwa ambacho makao makuu yake yatakuwa Mwanza, akisema miradi yote hiyo watashirikiana na JWTZ ili izidi kuwa endelevu.

Wakati huo huo Katibu Tawala huyo alimkaribisha rasmi mkuu mpya wa Jeshi la Uhamiaji Mkoa wa Mwanza, Kamishna Msaidizi, Kola Kayumba, anayechukua nafasi ya mtangulizi wake Kamishna Msaidizi Peter Mbaku anayehamia Mkoa wa Rukwa.



Katibu wa Kampeni Kitaifa ya Kupinga Ukatili wa Kijinsia na Ukatili kwa Watoto (SMAUJATA) Kanda ya Ziwa, Hashim Omary, akisalimiana na Mkurugenzi wa Shule ya Little English Medium ya mjini Shinyanga, Lucy Mfwele, wakati katibu huyo alipokutana na uongozi wa shule hiyo kuelezea umuhimu wa kampeni hiyo juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanafunzi waomba kujengewa uzio ili kudhibiti mwingiliano

**Na Halima Ikunji,** IGUNGA

WANAFUNZI wa kidato cha tano na sita kutoka Shule ya Sekondari ya Igunga mkoani Tabora wameiomba serikali iwasaidie kujenga uzio shuleni ili kudhibiti mwingiliano uliopo na jamii unaohatarisha usalama wao.

Walitoa ombi hilo juzi wakati wakizungumza na Nipashe na kueleza kuwa shule hiyo iliyopo jirani na makazi ya watu imekuwa na mwingiliano wa mara kwa mara hali inayohatarisha usalama wao na mali zao.

Mmoja wa wanafunzi hao, Laurine Munisi alisema kujengwa kwa uzio kutasaidia kuongeza usalama wa wanafunzi kuwa katika eneo salama tofauti na sasa ambapo usalama wao ni mdogo, kwamba wako hatarini kuvamiwa na vibaka muda wowote.

Alisema kwamba tahadhari ni muhimu sana kwao kwani hata wakianika nguo wanapata hofu ya kuibiwa kutokana na eneo hilo kuwa wazi na wakati mwingine kuhofu kuvamiwa na kujeruhiwa.

Naye Maganga Mohamed alisema shule hiyo kutokuwa na uzio kunasababisha baadhi ya wanafunzi wasiowaaminifu kutoroka na wengine kushindwa kusoma na kutekeleza wajibu wao ipasavyo.

Mwanafunzi mwingine, Ekilia Michael alimwomba Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kuwaongezea idadi ya mabweni kwani kwa sasa kuna baadhi ya wanafunzi wanalala wawili kwenye kitanda kimoja kutokana na wingi wa wanafunzi kulinganisha na mabweni yaliyopo.

"Pia hatuna bwalo la kulia chakula maana tunalia chakula chini ya miti hali inayoweza kusababisha mlipuko wa magonjwa," alisema Ekilia.

Mwalimu Mkuu Msaidizi katika shule hiyo, Wilson Manazi aliishukuru serikali kwa kuipatia shule hiyo fedha zaidi ya Sh. milioni 200 kwa awamu tofauti na kusaidia kujenga madarasa 12 pamoja na matundu ya vyoo.

Ofisa Elimu Takwimu, Mapambano Manyamvu alikiri uwepo wa adha zilizoainishwa na wanafunzi hao na kusema uwepo wa shule hiyo mjini inahitaji kuwa na uzio kutokana na mwingiliano uliopo.

Alisema shule hiyo ndiyo inayofanya vizuri kuliko zingine katika matokeo ya kidato cha nne na sitia, akisema kwa mwaka 2023 ilishika nafasi ya kwanza katika mtihani wa kidato cha sita kwa kufaulisha wanafunzi wote na watatu walipata daraja la pili.

Alisema mpaka sasa halmashauri imeweka utaratibu wa kushirikisha jamii, kuhakikisha uzio katika eneo hilo unajengwa ili shule na wanafunzi wawe na usalama.

## Wakulima 12,000 wajiandikisha kupata pembejeo

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKULIMA zaidi ya 12,475 kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga wamejiandikisha kupata pembejeo za ruzuku.

Ofisa Kilimo wa halmashauri hiyo, Richard Herege, aliyabainisha hayo wakati wa ukaguzi wa kituo cha kisasa cha rasilimali za kilimo kilichopo Kata ya Mwendakulima kilichofadhiliwa na mgodi wa Barrick Buzwagi.

Kituo hicho kitakuwa kinatumika kuwaelimisha wakulima namna ya kulima kisasa, uvunaji na kutafutiwa masoko ya mazao yanayopatikana.

Alisema miaka ya nyuma wakulima wengi walikuwa wanalima bila kufuata utaratibu ikiwa ni pamoja na kutokutumia mbolea za kukuzia, kupandia na kunenepesha hali iliyokuwa ikishusha uzalishaji katika kilimo.

Herege alisema msimu uliopita waliandikisha zaidi ya wakulima 9,000 na uzalishaji wa mazao uliongezeka na msimu huu wameongezeka hadi kufikia 12, 475 na sasa wanawatembelea kwenye mashamba yao na kuwapatia elimu ya muda gani waweke mbolea hizo ili kupata mavuno bora.

"Manispaa hii ina kata 20 kati ya hizi 12 wananchi wake wanajihusisha na kilimo cha mazao ya chakula, biashara na mikunde na awali walikuwa wakilima kienyeji bila kutumia pembejeo na kupata mavuno kiasi kwa kulima maeneo makubwa ambayo asilimia kubwa yalitumika kama chakula cha familia tu," alisema Herege.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, aliwataka maofisa ugani kila kata kutokutaa ofisini na badala yake wahakikishe wanawatembelea wakulima na kuwapatia elimu ya kulima kisasa, uwekaji wa mbolea za kukuzia, kupandia na kunenesha ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara.

Alisema msimu huu umekuwa na mvua nyingi kulinganisha na misimu iliyopita, hali inayowafanya wakulima kushindwa kujua nini cha kufanya shambani hivyo wanahitaji utaalamu wa kilimo.

ama
AFYA NA MAZINGIRA
ALHAMISI JANUARI 4, 2024



Ukurasa 14

## Taasisi inapoingia ubia na polisi kukabili vifo ajali



## 2024 na sura mafanikio sekta ya maji, Benki Dunia ikipiga makofi

Ukurasa 13

# Bingwa aibua yaliyojificha kuhusu ugumba, eneo kinamama hukosea

**Na Christina Mwakangale**

KWENYE jamii, wataalamu wa afya wanatoa wito wa kuachana na dhana potofu kuhusu ugumba, hususan kwa wanawake, kwa kuwa baadhi yao wanaangukia katika kinachoonekana kuwa kasoro.

Hivyo madaktari wanafafanua kwamba ni kundi la kuzaliwa na mji wa mimba wenye kasoro, zisizoweza kurekebishika hata kwa upasuaji.

Shirika la Afya Duniani (WHO), linasema mtu yeyote ambaye atashindwa kushika mimba kila anavyokusudia, huyo ni mgumba.

Pia ipo dhana katika baadhi ya mila nchini, mara tu msichana anapopevuka, huandaliwa sherehe ya kumtuza ikiwa ni ishara kwamba, binti yao amekua na ataanza kuziona siku zake kila mwezi na mara anapoolewa atashika ujauzito.




Bingwa wa Magonjwa ya Wanawake na Uzazi, MNH), Dk. Living Colman, anaweka tafsiri yake ni kwamba, ugumba ni hali ya mume na mke kushindwa kupata ujauzito kwa zaidi ya mwaka mmoja, bila ya kutumia uzazi wa mpango wowote.

Mtaalamu Bingwa wa Magonjwa ya Wanawake na Uzazi kutoka Chama cha Madaktari Bingwa wa Wanawake na Uzazi (AGOTA), Dk. Julius Kweyamba, anaendeleza ufafanuzi kwamba kimaumbile, mji wa mimba kutokuwa kawaida kwa mwanamke, ni miongoni mwa sababu zinazochangia kuwapo kinamama wagumba na wenye utasa.

“Mama huyu ameumbwa hivyo, mimba zinatoka, lakini watu wanakuwa na dhana kwamba huyu hutoa mimba.

“Maumbile hayo ni sababu ya ujauzito kutoka wenyewe. Nimeshakutana na baadhi ya ‘kesi’ (mikasa - mji wa mimba wenye kasoro) zipo zinazorekebishika na zisizorekebishika,” anasema Dk. Kweyamba.

Bingwa huyo ambaye ni Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha St. Francis cha Madaktari kilichopo Ifakara, anasema pamoja na ishara kuu na dhana iliyojengwa kwenye jamii kwamba mwanamke anayeona siku zake kila mwezi, uwezekano wa kushika ujauzito ni mkubwa, bado zipo kasoro za kimaumbile.

Hapo anatoa maelezo ya kina hivi karibuni, kuhusu uzazi katika moja ya semina zinazotolewa na Wakfu wa Vyombo vya Habari Tanzania (TMF), kwa waandishi wa habari za afya nchini.

Anataja kuwapo aina sita za mji wa mimba kwa wanawake na kati ya hizo, tano huwa na kasoro, aidha zinaweza kutibika au kutotibika na kuwa miongoni mwa sababu za ugumba kwa mwanamama.

“Mji au kizazi kinatakiwa kuwa na uwazi wa kutosha kubeba mtoto. Lakini, kama ana kizazi kama kimegawanyika mara mbili, hakitaruhusu ujauzito kufikisha miezi tisa, unaangukia kuharibika.

“Wengine wana kipande tu cha kizazi ambacho hakiwezi kubeba mtoto na wapo ambao kizazi kina ukuta mnene na kutokuwapo nafasi ya mtoto kukua.

“Lakini, wapo ambao shingo ya kizazi haistahimili kukaa miezi tisa, mimba zinatoka,” anasema Dk. Kweyamba na kuendelea: “Mwanamke anayeona ‘siku zake’ kila mwezi si hakikisho kwake, kwamba anaweza kushika ujauzito kwa asilimia 100.

“Kuna aina sita ya mji wa mimba na kati ya aina hizo mmoja tu ni upo sawa, zingine zinaweza kuwa na kasoro za kuzaliwa nazo na kuna uwezekano wa kurekebisha kwa upasuaji.

“Ingawa kasoro zingine hazirekebishiki na mwanamke huyo hataweza kupata mtoto kwenye maisha yake yote, jamii isidhani tu mwanamke aliyeolewa hapati ujauzito na kumlaumu, ikumbukwe kuna waliozaliwa mji wa mimba una kasoro na hazirekebishiki,” anasema Dk. Kweyamba.

**MIZIZI YA TATIZO**

Bingwa wa Magonjwa ya Wanawake na Uzazi MNH, Dk. Living Colman, anasema ugumba ni hali ya mume na mke kushindwa kupata ujauzito kwa zaidi ya mwaka mmoja, bila ya kutumia uzazi wa mpango wowote.

“Mzizi wa 'infertility' inategemea na chanzo, kwa mwanamke chanzo kikuu ni ‘hormonal imbalance' (mayai kushindwa kupevuka kwa mpangilio) na hii inaweza kutokana na ‘genetics’ (urithi), pia ulaji mbaya, sukari nyingi na mafuta husababisha unene uliopitiliza.

“Pia kupungua sana uzito (anorexia nervosa) inaweza kusababisha ugumba. Mirija kuziba ndio sababu ya pili ya ugumba kwa mwanamke na hii husababishwa na ngono zembe kama nilivyoeleza.”

Mtaalamu huyo anasema kwamba kwa mwanaume, sababu ya ugumba inaweza kutokana na kushindwa kuzalisha mbegu, sababu kuu ni mambo mbalimbali, ikiwamo ulevi kupindukia, sigara pia ulaji mbaya, sukari na mafuta pia kuziba kwa mirija inayopitisha mbegu inayosababishwa

Inaendelea Uk. 12

MAZINGIRA

## MRADI UNAKAMILIKA DESEMBA MWAKA HUU…

# Sh. bilioni 204 kuneemesha maji Korogwe, Pangani na Muheza



Shughuli za kutandika bomba kwenye mradi wa maji unaoendelea wilayani Handeni. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Hamida Kamchalla, TANGA**

MTU anapokuwa mkoani Tanga na kuitaja miji ya Korogwe, Handeni, Pangani na Muheza, hapo anaorodhesha ngome zake. Sasa kuna jipya katika hilo, wananchi wake wanatarajiwa kunufaika na kikubwa cha maendeleo ya maji, kinachofahamika 'Mradi wa Maji wa Miji 28.'

Ni mradi wa gharama kubwa, unaotarajiwa kutekelezwa nchini na serikali, kukitarajiwa kuwaondoshea kero za muda mrefu wananchi wake.

Ni fedha za mkopo gharama nafuu kutoka serikali ya India, kiasi cha Dola za Marekani milioni 500 (Sh.259 892 500 000) zimetolewa kwa ajili ya kutekeleza mradi wa maji wa miji 28 nchini.

Hadi sasa, Mamlaka ya Majisafi Handeni - Trunk Main (HTM), ni sehemu ya utekelezaji mradi wa miji 28, katika matarajio ya kuhudumia miji minne, ambayo ni Handeni, Korogwe, Muheza na Pangani.

Mkurugenzi Mtendaji wa HTM, Mhandisi Yohana Mgaza, anaiambia Nipashe kwamba kwa upande wa miji ya Korogwe, Handeni, Pangani na Muheza, mradi inaatarajiwa kugharimu Dola za Marekani milioni 81 (204,102,585,000/ Shilingi bilioni 204.102).

"Ni mradi mkubwa ambao tunategemea kuusimamia kwa makini, ni fedha nyingi sana ya serikali itatumika katika kuutekeleza hadi kumalizika na mradi huu utakuwa na chanzo kimoja tu, ambacho ni Mto Pangani," anafafanua.

Mhandisi Mgaza anaendelea: "Kutoka Mto Pangani, maji yatachukuliwa kwenye eneo la kijiji cha Mswaha Darajani yatasafirishwa mpaka kijiji cha Tabora kutakakojengwa mtambo wa kisasa kuchuja maji.

"Baada ya hapo ndipo maji yatatawanywa kwenda maeneo mbalimbali katika Miji ya Handeni, Korogwe, Pangani na Muheza kutakokojengwa matangi makubwa kwa ajili ya kuhifadhia maji hayo."

Katika Mji wa Handeni, anaeleza kutajengwa tangi lenye ujazo wa lita milioni mbili; Muheza tangi la lita milioni mbili; Pangani kutajengwa matangi ya ujazo lita 500,000 kijiji cha Boza, lita 300,000 kijijini Madanga na tangi jingine la lita 200,000 kujengwa kwenye kijiji cha Ubangaa.

Inafafanuliwa kwamba, mradi wote kwa ujumla wake utakuwa na urefu wa kilomita 189 kutoka kwenye chanzo cha maji, mpaka kufika penye matangi yanayoenda kuwahudumia wananchi waliko.

Mkurugenzi Mtendaji huyo, anaeleza kwamba kwa kuanzia, yatajengwa mabomba ya kusambaza maji yenye urefu wa kilomita 100 kufika maeneo yote ya miji na baadaye kazi ya usambazaji maji kwa wananchi itaendelea.

**UFANIKISHAJI MRADI**

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mgaza, kampuni zitakazoendesha ujenzi na kusimamia zote ni kutoka nchini India.

Nchini, mamlaka ya HTM inabakia kuwa wataalam wa Wizara ya Maji, wakiwa wasimamizi wanaohakikisha mradi unajengwa kwa viwango, ambavyo umefanyiwa usanifu kazi, hapo Mhandisi Yohana Mgaza akiahidi ufuatiliaji makini.

Katika tafsiri kuu inaelezwa mradi unatarajiwa kuhudumia zaidi ya watu 600,000 kwenye miji hiyo minne, huku wananchi watakaokuwa vijiji vilivyo umbali usiozidi kilomita 12 kutoka bomba kuu litakapokuwa linapita, nao wanatarajiwa kunufaika.

Kwa mujibu wa Mhandisi Mgaza, mkandarasi huyo hadi sasa yuko eneo la mradi akiendelea na kazi ya kulaza mabomba kwenye maeneo mbalimbali, kukiwapo ufafanuzi kuna kipande cha kutoka tangi la Korogwe mjini kuelekea kijiji cha Tabora penye chujio ndio ulazaji bomba umeanza.

"Pia, mkandarasi ameanza kulaza bomba kutoka kijiji cha Komsala kuelekea kijiji cha Mandela na kutoka Mandela, kuelekea kwenye kijiji cha Masatu.

"Mengine yamelazwa kwenye kijiji cha Tabora kuelekea mji wa Korogwe, huku ujenzi wa matenki ukiwa umeanza na yapo katika hatua ya kumwaga zege katika kijiji cha Madanga na Boza wilayani Pangani," anafafanua.

Mhandisi Mgaza anaendelea kueleza kwamba kazi ya kusafisha maeneo inaendelea ili ujenzi kuanza rasmi, ambapo ujenzi wa tenki la vibaoni, wilayani Handeni ukitarajiwa kuanza ikiwa ni pamoja na kusafisha eneo la kujenga chujio katika kijiji cha Tabora.

"Usafishaji unaendelea eneo la kujenga chanzo kijiji cha Mswaha, " anaeleza, akitamka ya ziada kuwa: "Sisi kama wataalamu wa HTM tukiwakilisha Wizara ya Maji, hatutakuwa kikwazo, tutahakikisha mradi unajengwa kwenye viwango stahiki na kukamilika kama ulivyopangwa."

Kuhusu ushirikishaji wananchi kwenye mradi, Mhandisi Mgaza, anasema kabla ya utekelezaji wake kuanza, walishirikiana na viongozi wa vijiji, kata, tarafa na serikali kupitia maeneo yatakayoguswa na mradi.

"Uhakiki wa wananchi wenye maeneo yenye mazao umefanyika ili kufidiwa na kusikokuwa na mazao wameombwa, ili kuweza kufanikisha kufika kulikokusudiwa," anabainisha.

Mradi huo ulioanza Aprili mwaka huu na unatarajiwa kukamilika ifikapo Desemba mwaka huu, tofauti na mtazamo wa awali kwenye usanifu wa Desemba 2025.

Hayo yamejiri, baada ya kuonekana umuhimu na mahitaji makubwa kwenye maeneo ya wananchi ambayo HTH, iliketi na wataalamu washauri na makandarasi kupitia mpango kazi wa utekelezaji na hivyo kujiwekea malengo mapya.

Kimsingi, mradi huo unoagusa wilaya nne za mkoani Tanga unaonekana kuwa fursa ya wananchi kujikwamua kiuchumi kwa kwenye maeneo yanayopitiwa na jirani, huku Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, ambaye ni mbunge wa wilaya mojawapo, akiwa na mchango mkubwa.

Malengo yaliyoko yanayotajwa ni kwamba, kipaumbele kitatolewa kwa wenyeji kushiriki shughuli za mradi, vijana wakihamasishwa kujitokeza, huku Mhandisi Mgaza akitaja lake kwamba kinamama wanaweza kujitokeza kwa biashara kama za chakula.

**Mawasiliano ya simu: +255 712336909.**

# BINGWA AIBUA YALIYOJIFICHA KUHUSU UGUMBA, ENEO KINAMAMA HUKOSEA

**INATOKA UK. 11**

na maambukizi ya magonjwa kama PID.

"Tiba ya ugumba ni kumuona mtaalamu wa afya (gynecologist) ambako atafanya vipimo na kugundua tatizo, halafu atatoa tiba husika. Kama ni 'hormonal imbalance' atapewa dawa na ushauri. Kama mirija imeziba atashauriwa apandikize (IVF).

"Si kweli kwamba matumizi ya dawa za uzazi wa mpango ndio chanzo cha ugumba. Ikiwa zitatumika kwa maelekezo ya mtaalamu, husaidia kuzuia mimba kwa muda fulani.

"Kuwapa watoto dawa za uzazi wa mpango ni kuwapa uhuru wa kufanya ngono zembe, hali inayosababisha kupata maambukizi kwenye uzazi (PID), hivyo kuathiri mirija ya uzazi na kushindwa kupata ujauzito," anatamka.

Mtaalamu huyo mwandamizi wa afya ya kinamama, anasema kwenye jamii hasa mijini, wengi wanatumia njia uzazi wa mpango wa dharura (emergency contraceptive pills) maarufu P2, akiitaja si sahihi kwa kuwa, ikitumika kila mara, inapoteza maana yake.

Bingwa huyo anashauri watoto wafundishwe kuepuka ngono za mapema, ambazo ndio chanzo cha maambukizi kwenye mifumo ya uzazi, hata inasababisha kuziba mirija na kushindwa kupatikana mimba.

MAZINGIRA

# 2024 na sura mafanikio sekta ya maji, Benki Dunia ikipiga makofi

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

SEKTA ya maji kitaifa sasa inaangukia katika mtazamo wa mafanikio ya uhuru kitaifa, kukihesabiwa miaka 62.

Iliko Tanzania sasa ni katika nchi 50 za mfano bora duniani, katika hatua za kuendeleza sekta ya maji, hata nyinginezo kukaribishwa kujifunza kinachotendeka.

Kupitia Programu ya Lipa kwa Matokeo (PforR) Wizara ya Maji imetekeleza zaidi ya miradi ya maji 1,500 iliyokamilika na inatoa huduma kwa wananchi.

Ikumbukwe serikali ya Tanzania imepanga kufikia lengo la upatikanaji huduma ya majisafi kwa asilimia 85 vijijini na mijini kwa asilimia 95.

Ikirejewa mapinduzi yanayofanyika katika miradi ya Sekta ya Maji hadi mwezi Desemba mwaka juzi, hali ya upatikanaji huduma ya maji nchini ilikuwa, asilimia 88 mijini na vijijini asilimia 77, kwa mujibu wa takwimu za Wizara ya Maji.

Ni kauli inayotoka kwa Makamu Rais wa Benki ya Dunia Kanda ya Mashariki na Kusini mwa Afrika, Dk. Victoria Kwakwa, Novemba mwaka jana.

Ilikuwa katika Mkutano wa Viongozi wa Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika, unaohusu upatikanaji majisafi na salama na usafi wa mazingira nchini Ethiopia, akipongeza Tanzania kwa mafanikio.

Hapo akataja ubora na viwango vya Programu ya Uendelevu wa Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (PforR), nchi ikawa kinara kiwango cha dunia, katika orodha ya nchi 50 duniani.

Dk. Kwakwa anaitaka Tanzania kutoa uzoefu wa mafanikio yake kwa nchi zaidi ya 23 Mashariki na Kusini mwa Afrika, zilizoshiriki mkutano huo muhimu.

Hivi karibuni katika ziara yake kikazi mkoani Singida, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akashuhudia huduma ya majisafi ilivyoleta mabadiliko katika maisha ya wananchi na kusukuma maendeleo.

"Tunang'aa na kupendeza na hapana shaka huduma ya maji nayo imeleta mabadiliko, sijaona madumu tupu wakati nikipokelewa," anatamka Rais Dk. Samia.

Programu ya PforR katika huduma za maji, ni mpango ulioanzishwa na Benki ya Dunia (WB) na kuanza kutekelezwa tarehe Julai mwaka 2019, kuhakikisha uhakika, usalama na mazingira vijijini.

Malengo yake yanatajwa kuchochea kasi ya utekelezaji Mpango wa Uboreshaji Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira, ikiweka motisha kwa viashiria, zilivyowekwa.

Pia miezi michache iliyopita, Rais Dk. Samia, akazindua mradi mkubwa wa maji wa Tinde -Shelui, unaotumia chanzo cha maji cha Ziwa Victoria, ukiwa na thamani ya shilingi bilioni 24.47, fedha zake zikiwa mkopo nafuu kutoka Benki ya Exim ya India.




Shughuli za kuzindua mradi wa maji, uliofanywa na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango. Picha nyingine ni tangi la maji. **PICHA: MTANDAO**

Mradi wa Maji Tinde – Shelui awamu ya kwanza, ulikamilika mnamo Agosti, mwaka jana kwa shilingi bilioni 24.47 na wananchi zaidi ya 40,000 wa vijiji vya Tinde mkoani Shinyanga na Shelui, Singida wakapata majisafi na salama; awamu inayofuata inatarajiwa kugharimu shilingi bilioni 16.2.

Hivi sasa, takwimu za Wizara ya Maji zinaonyesha vijiji 12,314 vinapata huduma ya maji bombani na 2,643 vimo njiani kunufaika ndani ya miezi 24.

**WAZIRI JUMAA AWESO**

Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, akizungumza na Nipashe, anasena ni matokeo ya Tathmini ya Hali ya Upatikanaji Maji Vijijini, iliyofanywa na Wizara ya Maji.

Anatamka kuwapo mabadiliko makubwa vijijini tangu kuanzishwa kwa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA).

Waziri anasema Wizara ya Maji imefanikisha huduma hiyo ya maji kwa visima na mabwawa kuchimbwa maeneo yote yenye uhitaji, kwa sababu kuna vifaa vya kazi hiyo na vinasambazwa nchi nzima.

Aweso, anataja mradi mkubwa wa sasa wa miji 28 wa thamani Dola za Marekani milioni 500, unaendelea kutekelezwa katika maeneo tofauti akiutaja ni matunda ya ziara ya Rais Dk. Samia nchini India hivi karibuni, akiahidi unakamilika mwaka ujao, 2025.

"Naipongeza Wizara ya Maji chini ya Waziri Jumaa Aweso kwa kazi nzuri inayofanyika huku na ninawahakikishia wananchi kuwa mradi huu mkubwa wa maji, hautaacha mji hata mmoja kati ya miji yote 28," anatamka Rais.

Nchini kunatajwa kuwapo maji mita za ujazo bilioni 126, kiasi cha kumhudumia kila mtu ni wastani mita za ujazo 2,105 kwa makadirio ya wakazi milioni 59.8 waliopo Tanzania Bara, kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022.

Hicho kinatajwa ni kiwango kinachotajwa, kuwa juu ya wastani wa mita za ujazo 1,700 kwa mtu kwa mwaka, kinachokubalika kimataifa.

Takwimu zinaonyesha nchini, kunatarajiwa kufikia kiwango cha wastani mita za ujazo 1,700 kwa mwaka, ifikapo mwaka 2030.

Hadi sasa kunatolewa angalizo, suala la uhitaji wa kuwapo usimamizi na uendelezaji rasilimali za maji ni muhimu jamii ziliko.

Takwimu za Wizara ya Maji, zinaonyesha kuwa hadi kufika Aprili 2023, kulikuwapo jumla ya vituo 136 vilivyorabatiwa kufuatilia rasilimali maji na vingine zaidi ya 2,000 vya majukumu mbalimbali ya maji, katika hatua ya ujenzi na majukumu mbalimbali ya maji.

Mtaalamu wa Benki ya Dunia, Esha Zaveri hivi karibuni ananena kuwa asilimia 60 ya watu duniani hupata janga la uhaba wa maji na miongoni mwa vichochezi vya janga hilo, anataja ni kuongezeka idadi ya watu na shughuli za kibinadamu katika vyanzo vya maji.



AFYA

# Taasisi inapoingia ubia na polisi kukabili vifo ajali za barabarani

## • Yakusanya wadau kimataifa kuumiza kichwa...

**Na Halfani Chusi**



Wadau wa Usalama Barabarani waliokutana jijini Mwanza hivi karibuni, kujengeana uwezo kuhusu masuala ya usalama barabarani. Kulia ni Mkurugenzi wa Taasisi ya Mpango wa Usalama Barabarani (TARSI), Maliki Barongo, ambao ndio waandaaji wa semina hiyo. **PICHA: HALFANI CHUSI**

INAGEUKA nadharia dhahiri kila kunapokucha, kuna watu wanaopata ulemavu wa kudumu, kuongeza wategemezi kijamii, hata yatima na wajane, kisa na mkasa ni ajali za barabarani.

Ni hali inayoendana na wanafunzi kukatisha masomo kwa kuondokewa na waliokuwa wanawategemea kwa malipo ya matunzo, ada, kuharibika miundombinu, pia kupunguza nguvukazi ya taifa na kuharibika chombo cha moto, mmiliki anaingia hasara ya matengenezo.

Ni matukio yanayoigusa Taasisi ya Mpango wa Usalama Barabarani (TARSI), hata wakaamua kubeba ajenda ya kutoa elimu kwa wamiliki wa vyombo vya moto na madereva wao.

Mzizi wa elimu hiyo inaanzia shuleni kwa wanafunzi wakiwakumbusha mpaka wa watembea kwa miguu, elimu ya kuzifahamu sheria za barabarani na hata kuvuka mpaka kimataifa kwa kuendesha semina.

Wilayani Kinondoni, ambako ndiko masikani ya TARSI, tayari baadhi ya shule zimefikiwa na 'shule' hiyo, pia madereva na wamiliki wa vyombo vya moto, wakiamini elimu ikianzia ngazi hizo, kutafikiwa azma ya lengo kufutika ajali na vifo.

Taasisi hiyo inafika mbali, baada ya kuwakutanisha wataalamu na wadau usalama barabarani, wakapeana uzoefu wa usalama na namna ya kutekeleza sheria na taratibu za yanayotumika barabarani, ili kudhibiti ajali zinazochangiwa kwa kiasi kikubwa na sababu za kibinadamu.

Wadau wanaotajwa wanaotoka nchi za Kiafrika kama vile; Afrika Kusini, Rwanda, Burundi, Botswana na wenyeji Tanzania walikungana jijini Mwanza kwa semina ya siku tano kubadilishana uzoefu na mbinu za kukabiliana na ajali za barabarani.

### NAIBU WAZIRI

Hiyo ikawahusisha wataalamu kutoka nchi hizo na wasimamizi wa sheria za usalama barabarani nchini, zikipambwa na hoja nzito kitaalamu, kwa mustakabali wa kumaliza ajali za barabarani nchini na ilifunguliwa na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Jumanne Sagini.

Kwenye ufunguzi, Sagini anasema vifo vitokanavyo na ajali za barabarani nchini, kwa mujibu Shirika la Afya Duniani (WHO), mwaka 2018 vilikiwapo 16,000, hapo akasisitiza imani yake kwa mafunzo hayo yataboresha huduma na taratibu za matumizi ya Barabara, kwa sababu wanapata fursa kujifunza mengi na uzoefu kutoka nchi zingine zinazoendelea.

"Ajali za barabarani zinatokana na sababu za kibinadamu ambayo ni ya dereva mwenyewe, pia kuna matatizo ya vyombo vya moto vyenyewe, uchakavu na ubovu pamoja na miundombinu kuwa mibovu, ambayo inachangia kwa kiasi kikubwa hivyo warekebishe.

"Tunaona kila siku Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani nchini, Ramadan Ng'anzi, akiwaeleza Watanzania na watumiaji wengine wa barabara juu ya sheria na taratibu za utekelezaji wa shughuli zinazotumia barabara, lakini ajali zinaendelea kuwapo," anafafanua Sagini.

### WENYEJI MKUTANONI

Mkurugenzi Mtendaji wa TARSI, mwenyeji wa kuandaa semina hiyo, Maliki Barongo, anasema kazi yao kubwa ni kutoa elimu ya usalama barabarani kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

Anaeleza kuwa, elimu hiyo wanaanza kutoa kwa wasanifu wanaojenga barabara mpaka watumiaji wa mwisho, ambao ni watembea kwa mguu, lengo ni kuhakikisha nchi inakuwa salama na kuepukana na ajali za barabarani.

"Lengo kubwa la semina hii, ni kubadilishana uzoefu wahandisi wa nchini hapa na kutoka nchi zilizoendelea katika usalama barabarani pamoja na Jeshi la Polisi nchini, kujifunza kutoka nchi zingine," anatamka Barongo na kuendelea:

"Sambamba na kutambua mapungufu kama shida ni kwa wajenzi, wasanifu au watungaji sheria ili mwisho wa siku, wapate kitu kitakachoweza kusaidia kupunguza ama kumaliza ajali za barabarani hapa nchini."

Kamanda wa Kikosi cha Polisi Usalama Barabarani nchini, Ramadhani Ng'anzi, anaitaja Tanzania imo katika nchi tatu ukanda wa Afrika Mashariki, zinazotajwa kupunguza ajali za barabarani, baada ya kuwekwa mifumo madhubuti, ikiwamo uboreshaji miundombinu ya barabara.

Anasema nchi ina sheria, kanuni na taratibu za kupambana na ajali hizo, japokuwa bado zipo zinazotokana na miundombinu mibovu, makosa yanayosababishwa na madereva kwa kutofuata sheria na ubovu wa magari.

"Tumekutana kuyachanganua na mwisho wa siku ndoto ya Tanzania bila ya ajali, inawezekana iweze kutimia, hakika tunaendelea vizuri na tangu Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani aruhusu mabasi yasafiri usiku, sasa hivi ni mwezi wa pili hatujasikia basi limepata ajali.

"Zimetokea ajali mbili kubwa hivi karibuni na zote zimetokea mchana, tunajitahidi kuangalia kwanini ajali zimetokea mchana lakini usiku hazijatokea hivyo imekuaje usiku wameweza," anaeleza Ng'anzi.

Dk. Amon Mwasandube ni Mhadhiri wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji, ni mshiriki wa mafunzo hayo, anayeeleza kuwa barabara zinachangia kusababisha ajali kwa kiasi kikubwa, pia sheria, taratibu na kanuni zinatakiwa kila mara zihuishwe, kutokana na teknolojia inavyobadilika.

Mkuu wa Idara ya Mipango TANROADS, Mkoa wa Mwanza, Mhandisi Magesa Mwita, anasema barabara wanazojenga wanazingatia suala la usalama na akasisitiza wanazipaka rangi na kuweka alama za barabarani na zinapofifia, huwa wanafanya jitihada kurudishia, ili watumiaji wake wazifuate bila ya matatizo.

### MADEREVA WALONGA

Dereva wa Basi la New Force, Festo Juma anasema, hatua ya utoaji wa elimu kwa usalama barabarani ni nzuri, lakini sababu kubwa ya ajali ni ufinyu wa barabara kwa baadhi ya maeneo.

"Serikali inajitahidi sana kupunguza ajali kwa kutoa elimu, lakini shida kubwa kuna sehemu barabara ni finyu nyembamba, inabidi ifanyike jitihada ya kuzipanua ziwe mbili zinakwenda mbili zinarudi, kama ilivyo kwa barabara za Ubungo - Kimara (Dar es Salaam).

"Nchi nzima ingekuwa ipo kwa namna hiyo, ajali zisingetokea, mfano hizi ajali za kugongana uso kwa uso zingekuwa hazipo kabisa kwa sababu gari zinazoenda na zinazorudi hazipishani.

"Kingine, kuna baadhi ya sehemu kuna mashimo kwenye barabara amabayo hayajarekebishwa, sasa dereva akiliingia kwa bahati mbaya, inaweza kutokea ajali kwa hiyo lazima miundombinu ya barabra iangaliwe kwa upana mkubwa sana," anashauri Juma.

Dereva mwingine anayefanya safari zake kati ya Iringa na Dar es Salaam, Salumu Chauya, anashauri kila basi la abiria hasa katika kipindi cha sikukuu, awe anapanda askari walau mmoja wa usalama barabarani kufuatilia uendeshaji wa dereva, awapo kinyume amkemee.

"Mimi ninaona huo ungekuwa utaratibu mzuri sana, kwa sababu dereva akijua ndani ya gari yupo askari, atatii sheria zote za barabarani. Ninaamini kwa kufanya hivyo tutapunguza ajali kwa kiasi kikubwa sana.

"Ajali nyingi zinatokea kwa madereva wengi kushindwa kuzingatia sheria kwa uzembe kwa sababu wengi wamesoma na wanazijua, kwa hiyo inahitajika nguvu kubwa sana kwenye kukabiliana na ajali za barabarani," anashauri Chauya.





# Wakulima wapewa mbegu za majaribio

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SHIRIKA la Wakulima na Wazalishaji wa Mbegu Dodoma (DASPA) limetoa kilo 150 za mbegu za karanga kwa wananchi kwa lengo la kufanyiwa majaribio, kisha kutoa mrejesho wa namna zinavyoota na kuvumilia ukame na magonjwa.

Katibu Mtendaji wa shirika hilo, Aithan Chaula, aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa.

Chaula, alisema kuwa jumla ya kilo 150 za mbegu za karanga aina ya Naliendele 2016, nari nut 2015, na nachi 2015 zimetolewa kwa wakulima waliotembelea maonesho ya Nanenane mwaka huu.

Alisema lengo ni wananchi wakiwamo wakulima wakapande katika maeneo yao na kuona jinsi karanga hizo zinavyoota, zinavyovumilia ukame na magonjwa na watawafuatilia ili kupata mrejesho.

Alisema kuwa wananchi wengi waliotembelea maonesho hayo walitaka kujifunza kuhusu kilimo cha karanga na teknolojia mbalimbali.

Alisema katika maonesho hayo waliwaonyesha wananchi

teknolojia mbalimbali ikiwamo mashine za kupandia, mashine za kulimia (power tiller) mashine za kupukuchulia karanga na nyinginezo.

Naye Mwenyekiti wa DASPA, Janeth Wilson, alisema kwa sasa mwamko kwa wananchi juu ya masuala ya kilimo umeongezeka.

Alisema: "Wananchi wengi wanapenda kujua kilimo cha kutumia teknolojia na hata matumizi ya mbegu bora ni jambo linalotia moyo kuona kwamba kilimo kinapewa msukumo zaidi na wananchi."

**Katibu Mtendaji wa shirika hilo, Aithan Chaula, aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa.**

# Mfumo wa kudhibiti mbegu feki waanzishwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

TAASISI ya Kudhibiti Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI), imeweka mfumo bora wa kudhibiti mbegu 'feki' kwa kutumia lebo ya kielektroniki.

Mkurugenzi Mkuu wa TOSCI, Patrick Ngwediagi, alisema hayo wakati wa mkutano mkuu wa mwaka wa Chama cha Sayansi ya Kilimo na Mazao Tanzania (CROSAT).

Mkurugenzi huyo ambaye ni Katibu Mkuu wa CROSAT alisema kuwa katika kuhakikisha wanadhibiti uwepo wa mbegu feki hivi sasa kuna utaratibu wa udhibiti wa kutumia lebo za kielektroniki za TOCSI.

"Unaponunua mbegu kuna sehemu ya kukwangua utakutana na taarifa inayokupa maelekezo kuwa mbegu hiyo ni halali," alisema.

Kutokana na hali hiyo aliwataka wakulima kutumia mbegu bora ili wapate mazao bora.

Alisema baadhi ya wakulima wamekuwa wakitoa visingizio kuwa mbegu bora ni gharama.

"Wengi hawatumii mbegu bora kwa kisingizio cha kuwa ghali, wanatakiwa kutambua kuwa mbegu bora inalipa kwani unaweza kulima eneo dogo na kupata uzalishaji mkubwa," alisema.

Alisema matumizi ya mbegu ambazo si bora yanasababisha wakulima kulima mashamba makubwa na kisha kupata mavuno kidogo," alisema.

Kadhalika alisema kuwa mbegu bora zinazotumika nchini zimefanyiwa utafiti na wakulima wanatakiwa kufuata maelekezo ya matumizi ya mbegu ili kuwe na tija na ufanisi kwenye kilimo.

Mwenyekiti wa mkutano huo ambaye ni Rais wa Chama cha Wataalam wa Sayansi ya Mimea, Prof. Kallunde Sibuga, alisema katika mkutano huo mbali na kujadili mafanikio, mikakati na changamoto watapitia katiba ya chama hicho ambayo iko katika hatua za mwisho za maboresho.

Alisema kuwa pia wakati wa mkutano huo kutakuwa na semina ya kitaaluma ya kisayansi.

Kuhusu Chama cha CROSAT, alisema ni chama ambacho wanachama wake ni wakulima na mashirika ya wakulima, wahadhiri, watafiti, wakufunzi, maofisa ugani, vyombo vya udhibiti ubora wa kilimo mazao, wanafunzi na mashirika ya wanafunzi, taasisi zisizo za kiserikali, kampuni binafsi, watengenezaji, wasindikaji, na wauzaji wa mazao mbalimbali na bidhaa," alisema.

Alisema kuwa CROSAT ilizinduliwa rasmi mwaka 2022 na makao yake makuu yako Mkoa wa Morogoro.

Naye meneja wa ushauri wa majaribio ya viuatilifu kutoka Taasisi ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania (TPHPA), Prof. Eliningaya Kweka, alisema wakulima wanahitaji elimu zaidi juu ya matumizi ya viuatilifu.



Baadhi ya daladala zikiwa zimeziba barabara ya CDA jijini Dodoma na kusababisha magari mengine kushindwa kutumia njia hiyo kutokana na madereva hao kupakia abiria nje ya eneo la Nyerere Square wanapopakia abiria. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Askofu ataka mwaka 2024 uwe wa kuibua miradi ya kiuchumi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

NAIBU Katibu Mkuu Taifa wa Kanisa la Pentecostal Holiness Association Mission Tanzania (PHAM) (T), Askofu Julius Bundala, amewataka Watanzania kuutumia mwaka 2024 kufanya kazi kwa bidii na kuibua miradi mbalimbali ya kuwakwamua kiuchumi ili kuondokana na umaskini.

Bundala, alitoa kauli hiyo alipokuwa kwenye ibada ya kukaribisha mwaka mpya 2024 iliyofanyika kwenye Kanisa la Bethania Chinyoya Kilimani jijini hapa.

Askofu Bundala aliwataka Watanzania katika kipindi chote cha mwaka 2024, kutokuwa kikwazo cha kupata maendeleo na kujikwamua na hali ngumu ya maisha, badala yake watumie muda mwingi kujituma kwa bidii.

Alisema bado kuna shida kwa baadhi ya wananchi kuinyoshea vidole serikali kutokana na ugumu wa maisha wakati muda mwingi wanautumia kukaa vijiweni na majumbani badala ya kujishughulisha na kazi za kuwaletea kipato.

Alisema watu kama hao wamekuwa kikwazo kikubwa cha kukua kiuchumi kutokana na muda mwingi kutokufanya kazi ambazo zingewawezesha kubadilisha maisha yao kwenye familia husika.

"Nitumie nafasi hii ya kuukaribisha mwaka huu mpya wa 2024 na kuuaga mwaka 2023, Watanzania wafanye kazi zenye kutuletea kipato pamoja na kuibua miradi mbalimbali ikiwamo ya ufugaji, kilimo na mingineyo yenye tija" alisema.

Pia aliwataka vijana kujitengenezea miradi mbalimbali itakayowawezesha kujiajiri wenyewe badala ya kukaa majumbani na kusubiri kuletewa ajira.

Kuhusu elimu, Askofu Bundala aliwataka waliopo masomoni kuongeza bidii ili waweze kufanya vizuri kwenye elimu na hatimaye serikali na kanisa liweze kuwapata wasomi watakaoleta maendeleo nchini.





# Ekari 385 za mashamba zavamiwa na viwavijeshi

**Na Elizabeth John,**
LUDEWA

EKARI 385 za mashamba wilayani Ludewa Mkoa wa Njombe zimevamiwa na wadudu aina ya viwavijeshi na kuathiri mashamba yao.

Wakizungumza na Nipashe wakulima hao wamesema wameingiwa na hofu la janga la njaa kutokana na wadudu hao kuingia katika mashamba yao na kushambulia mazao na hivyo kuiomba serikali kuchukua hatua za haraka katika kuwadhibiti ili wasiweze kuleta athari zaidi.

Castory Luoga ni mkulima mkazi wa Ludewa, alisema kuwa wadudu hao ni tatizo kwa sababu wanaharibu mazao licha ya gharama kubwa ambayo wametumia katika kilimo.

"Mkulima ametumia gharama kubwa, amenunua mbegu, amelipa vibarua, amelipa wenye ng'ombe lakini inafika wakati unakuta wadudu wamechakaza kumekuwa kweupe," alisema Luoga.

Naye Ayubu Haule alisema kuwa viwavijeshi wameshambulia kwa kasi na wasipodhibitiwa kutakuwa na njaa kali. "Sasa wameshashambulia sehemu kubwa na mashamba mengine yapo tupu, kwa hiyo tunaiomba serikali kulingana na haya madhara yatakayotokea mwaka 2024 waangalie kipaumbele zaidi kwa sababu hili janga sio dogo," alisema Haule.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Nyamapinda, Francis Mwinuka, alisema wadudu hao wameshambulia mashamba ya watu yakiwa na mahindi ambayo wamegharamia mbolea na mbegu.

"Naomba kwenye serikali itoe msaada wa helikopta ili kusaidia kumwaga dawa ili hawa wadudu waishe kwa sababu kwa kutumia mabomba kila mmoja anapiga katika mashamba yake lakini hakuna mabadiliko kwa sababu wadudu wanazaliwa kila baada ya muda," alisema Mwinuka.

Ofisa Kilimo Wilaya ya Ludewa, Godfrey Mlelwa, alisema mnamo Desemba 23 mwaka 2023 kulitokea changamoto ya kuvamiwa na wadudu aina ya viwavi jeshi katika Kata ya Ludewa.

"Walianza kuvamia katika maeneo ya Nyamapinda na Mdonga kwa kasi kubwa sana na hawa viwavi ni wadudu waharibifu kwa sababu wanapojitokeza wanavamia mazao na kufanya uharibifu mkubwa na ni wadudu wanaotokana na unyeshaji mvua kidogo," alisema Mlelwa.

Alisema kwa upande wa eneo la Nyamapinda zaidi ya hekari 380 mashamba yaliyolimwa yamevamiwa na wadudu hao.

"Na kati ya hizo, hekari 280 ilikuwa ni eneo la mazao ya mahindi lakini hekari 100 ilikuwa ni eneo la mapori ambalo limeachwa wazi halijalimwa kwa hiyo na eneo lingine la hekari kama 100 ni eneo la Magereza kwa hiyo ni maeneo ambayo yalivamiwa na hao wadudu," alisema Mlelwa.

Alisema kuwa tayari serikali imeanza kuchukua hatua ambapo Wizara ya Kilimo kupitia taasisi inayojihusisha na afya ya mimea (TPHPA) imeweza kutoa dawa lita 1,000 ili kupambana na wadudu hao.



Mvua iliyonyesha jijini Dar es Salaam hivi karibuni imeharibu kingo za Mto Msigani uliopo Mbezi Luis na kusababisha nyumba zilizoko karibu na mto huo kuwa hatarini kubomoka- **PICHA: SABATO KASIKA**

# RC ahimiza kilimo cha mboga, ufugaji kupambana na udumavu

**Na Elizabeth John,**
NJOMBE

MKUU wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, amesema ili kupambana na udumavu ipo haja ya kila shule za msingi na sekondari mkoani humo kufanya kilimo cha mboga pamoja na ufugaji wa kuku wa mayai ili watoto wapate mlo kamili.

Mtaka aliyasema hayo katika uzinduzi wa mradi wa miaka mitano wa lishe mtambuka unaofadhiliwa na Serikali ya Marekani (USAIDS) wenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 800 kwa mwaka.

"Tutahitaji kupata taarifa za shule zetu zote za msingi na sekondari, shule zetu zinamaeneo makubwa kiasi gani ili tuangalie halmashauri ambazo ziko tayari wao wakubali kulipia vifaranga 1,000 kwenye shule fulani kwa ajili ya mradi wa kuzalisha mayai," alisema Mtaka.

Mtaka alisema hiyo itasaidia shule kuwa na mradi ambao utasaidia watoto kupata mlo kamili ili kupambana na udumavu.

"Halmashauri kwenye hela inayotenga Sh. 1,000 ya watoto wao wanaweza wakaamua kama halmashauri ni darasa lipi wakakubaliana watoto wapate mayai kama sehemu ya lishe," alisema Mtaka.

Msimamizi wa mradi wa lishe mtambuka, Dk. Joyceline Kaganda alisema mradi huo utakuwa ukitoa kuku wa mayai na mbegu za mazao lishe kwa shule ili kukabiliana na udumavu.

"Mradi utatusaidia kufundisha kinamama wetu jinsi ya kuandaa chakula kilichorutubishwa lakini na mahindi pia kwa sababu uhifadhi mbaya wa mahindi ndiyo unatuletea sumu kuvu kwa hiyo tunafanya kazi pamoja ili kuhakikisha mahindi yetu hayapati sumu kuvu kwa sababu utafiti unasema sumu kuvu inaongeza udumavu," alisema Dk. Kaganda.

Mkuu wa Wilaya ya Ludewa, Victoria Mwanziva, alisema kuwa udumavu upo na wanaukabili kwa kampeni mbalimbali za lishe haswa kwa mama na watoto.

Mkuu wa Wilaya ya Wanging'ombe, Claudia Kitta, alisema kuwa ili kupambana na udumavu wamekuwa wakitoa elimu kwa vitendo ikiwamo kufundisha ukorogaji wa uji lishe pamoja na unyonyeshaji.

# 'Uchimbaji wa visima utamaliza tatizo la upatikanaji majisafi'

**Na Elizabeth John,** LUDEWA

MENEJA wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mzingira Vijijini (RUWASA) Wilaya ya Ludewa Mkoa wa Njombe, Mhandisi Jeremiah Maduhu, amesema mpango wa serikali wa uchimbaji wa visima utasaidia kutatua tatizo la upatikanaji wa majisafi na salama kwa wananchi.

Maduhu aliyasema hayo katika Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ilipofanya ziara ya kukagua utekelezaji wa miradi ya maji wilayani hapa.

Alisema wazo la kuamua kuchimba visima virefu lilikuja baada ya kuona kwamba kuna baadhi ya maeneo ambayo yamekuwa na tatizo la upatikanaji wa maji juu ya ardhi.

"Kwa hiyo eneo hili tumekosa vyanzo vya mserereko ndiyo tukaja na wazo sasa la kuamua kuchimba hivi visima virefu, kimsingi tulifanya utafiti katika visima hivi vinne katika kila eneo na ripoti ya utafiti ilituelekeza kuwa tunapaswa kuchimba visima vyenye urefu wa mita fulani," alisema Maduhu.

Kwa upande wa Mkuu wa Wilaya ya Ludewa, Victoria Mwanziva, alisema ili kutatua changamoto ya upatikanaji wa maji safi na salama, Rais Samia Suluhu Hassan alinunua magari 26 ya dharura kwa ajili ya kuchimba visima nchi nzima.

"Kuna miradi ya muda mrefu na ya muda mfupi na gari moja la Mkoa wa Njombe lipo hapa wilayani Ludewa linaendelea kufanya kazi linachimba visima vya maji kwenye Kata ya Manda ili kuhakikisha kwamba tunapata huduma bora ya maji," alisema Mwanziva.

Diwani wa Kata ya Manda, Elfrida Kizota, alisema kazi ya uchimbaji wa visima itawasaidia wananchi kuondokana na tatizo la kufuata maji ziwani.

"Sisi tunasema katika suala hili la uchimbaji visima mama (Rais Samia Suluhu Hassan) ametuokoa sana, ametuepusha kwanza kutafuta maji kwa umbali mrefu, amemtua ndoo kichwani mwanamke na kupata maji safi na salama," alisema Kizota.

Maura Komba ambaye ni mkazi wa Kijiji cha Igalu, alisema hapo awali walikuwa wakichota maji katika ziwa ambalo halikuwa salama kwa afya zao kutokana na mito ya pembezoni kutiririsha maji ambayo yalikuwa na takataka.





## Waziri atoa tahadhari wanaojenga kando ya barabara

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba Sheria na Utumishi wa Umma, Haruon Ali Suleimani, ameitaka Serikali ya Mkoa wa Kusini Unguja, kuwazuia wananchi wanaojenga pembezoni mwa barabara ili kuepuka kuvunjiwa nyumba zao wakati wa utanuzi wa barabara.

Aliyasema hayo jana eneo la Cheju Wilaya ya Kati Unguja wakati wa ufunguzi wa Barabara ya Cheju Kibele ikiwa ni kuelekea maadhimisho ya miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Alisema barabara hiyo imejengwa kwa kiwango cha lami, ni rahisi kwa wananchi kujenga pembezoni mwa barabara bila kufuata utaratibu jambo ambalo wakati wa utanuzi wa barabara utapofika litawaletea matatizo.

Haroun alisema serikali ya mkoa na mamlaka husika wanapaswa kuwa karibu kuifuatilia barabara hiyo ili kuepuka hayo yasitokee.

"Hii barabara sasa ni mpya na eneo hili hili awali halikuwa na barabara lakini kwavile barabara hii imejengwa kwa kiwango cha lami bila shaka watajitokeza watu kujenga pembezoni mwa barabara," alisema.

Aidha aliwatahadharisha madereva kuchukuwa tahadhari na kutoendesha vyombo vyao kwa mwendo wa kasi na kuzingatia sheria za makosa ya barabarani ili kuepukana na ajali.

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Khadija Khamis Rajabu, alisema barabara hiyo yenye urefu wa kilomita 3.8 inajengwa na kampuni ya Uturuki iitwayo ASER na kusimamiwa na Taasisi ya Ujenzi na Wakala wa Barabara Zanzibar na kujengwa kwa utaratibu na makubaliano waliokubaliana.

Alisema zaidi ya Dola za Marekani milioni moja zitatumika kukamilisha ujenzi huo na ujenzi wake ulianza Oktoba 15 mwaka 2022 na kumalizika Janauri mwaka huu.

Mkuu wa Wilaya ya Kati, Sadifa Juma alisema kuwa barabara hiyo imejengwa kwa uwezo wa kupitisha magari yenye uzito wa tani 10 na kwamba gari zenye uzito zaidi ya huo haziruhusiwi kupita kwa sababu zitasababisha barabara kuharibika.

# Wanne mbaroni kwa kujeruhi, kufanya unyang'anyi Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

HALI ya taharuki imetanda kwa wananchi wa Zanzibar baada ya kutokea kwa matukio ya baadhi ya watu kushambuliwa na mapanga na watu wasiojulikana.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi, Richard Tadei Mchomvu, watu wanne wamejeruhiwa nyakati za usiku wakiwa majumbani mwao eneo la Mwanyanya na Dole mkoani hapa.

Alisema baada ya tukio hilo Jeshi la Polisi lilifanya msako na kufanikiwa kuwatia mbaroni watu sita wanaodaiwa kuhusika na tukio hilo.

Alisema watuhumiwa wengi wakiwa ni vijana wenye umri kati ya miaka 13 hadi 30 ambao wamekuwa wakiwashambulia watu kwa kuvunja milango ya nyumba.

Alisema katika msako huo pia walifanikiwa kupata runinga ambayo ilitelekezwa porini na wahalifu hao.

"Wahalifu hao walivunja nyumba za wananchi zipatazo sita na kuingia ndani kuwashambulia wananchi na kuwanyang'anya vitu mbalimbali ikiwamo simu 18, kompyuta mpakato moja, runinga moja na fedha shilingi 85,000," alisema.

Alibainisha kuwa katika tukio hilo wahalifu hao waliwajeruhi vibaya watu wanne kwa kuwakata na mapanga kichwani na kuwajeruhi sehemu mbalimbali za miili yao.

Kamanda Mchomvu alisema juhudi za kuwabaini na kuwakamata watuhumiwa wengine wa tukio hilo zinaendelea na upelelezi utakapokamilika watafikishwa mahakamani kwa mujibu wa sheria.



Washiriki wa Kongamano la Miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar lililoandaliwa na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo Zanzibar kwa ajili ya Baraza la Vijana na Taasisi za Wizara hiyo, wakisikiliza mada jana mjini Zanzibar. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# Mil.10/- zatolewa mkakati kuimarisha afya wawakilishi

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

BENKI ya NMB imekabidhi vifaa vya Sh. milioni 10 vitakavyotumika katika bonanza la michezo litakalowakutanisha wafanyakazi wa benki hiyo na wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar kwa lengo la kuimarisha afya zao.

Bonanza hilo litafanyika Januari 11, mwaka huu katika viwanja vya Mao Tse Tungi visiwani hapa, vifaa vilivyotolewa ni track-suit, jezi za mpira wa miguu, netiboli, mpira wa kikapu, mipira, medali na vikombe.

Akizungumza wakati wa hafla ya makabidhiano hayo, Mkuu wa Mtandao wa Matawi na Mauzo ya Rejareja wa Benki ya NMB, Donatus Richard, alisema bonanza hilo ambalo ni miongoni mwa maadhimisho ya kuelekea kilele cha sherehe za miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar linalenga kuhimiza michezo kama njia ya kuboresha afya kwa wawakilishi hao.

"Kama benki, tunaamini michezo ina mchango mkubwa katika kujenga miili yenye afya kwa wananchi, ndiyo maana tumekuwa tukiandaa mabonanza kama haya hapa visiwani Zanzibar na Tanzania Bara kwa zaidi ya miaka saba sasa. Tofauti na mabonanza tuliyofanya hapa visiwani miaka ya nyuma, mwaka huu tumewaalika wabunge kutoka Tanzania Bara kushiriki," alisema Richard.

Kadhalika alisisitiza dhamira ya benki hiyo kuendelea kushirikiana na wadau mbalimbali visiwani Zanzibar ili kuimarisha maendeleo ya sekta ya michezo.

"Uendelezaji wa sekta ya michezo unaweza kufungua fursa nyingi za ajira hasa kwa vijana. Kama benki, tutaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wa michezo ili kuhakikisha sekta hii inaendelea kupiga hatua," alisema.

Naye Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Zeuberi Ali Maulid, wakati wa hafla hiyo aliipongeza benki hiyo kwa kuendelea kuunga mkono mipango mbalimbali ya maendeleo visiwani Zanzibar, huku akisisitiza dhamira ya baraza lake kuendelea kufanya kazi kwa karibu na benki hiyo.

"NMB kupitia falsafa yake ya 'karibu yako' imekuwa ikifanya kazi kwa karibu sana na baraza letu. Tunafuraha kuwa benki leo imeendeleza uhusiano wetu kwa kutoa vifaa hivi vya michezo leo na tunaamini timu yetu itaibuka kidedea wakati wa bonanza hili," aliongeza.

Naye Mwenyekiti wa Timu ya Michezo wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Miraji Kwaza, alipongeza benki hiyo kwa kudhamini bonanza hilo, akieleza kwamba matumaini yake kuwa bonanza la mwaka huu litakuwa kubwa na bora zaidi.

Alisema: "Tunashukuru kwa vifaa hivi vya michezo vilivyotolewa na Benki ya NMB leo. Bonanza la mwaka huu limesheheni burudani nyingi na ninaamini litakuwa kubwa na bora zaidi".

Awali, Katibu wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Raya Issa Mselemu, alibainisha kuwa mbali na michezo benki hiyo imekuwa ikishirikiana kwa baraza lake katika masuala mbalimbali ya kimaendeleo.

# Polisi: Tukumbuke wazee wenye uhitaji

**Na Issa Mwadangala, SONGWE**

WAKAZI wa Mkoa wa Songwe wametakiwa kutoa msaada kwa watu wenye mahitaji maalum katika jamii kwa lengo la kuwafariji na kuwaweka karibu na jamii.

Msaidizi wa Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai Mkoa wa Songwe, Mrakibu wa Polisi (SP) William Nyamakomago alitoa kauli hiyo jana wakati wa hafla iliyoandaliwa na kikundi cha kuwasaidia watu wenye uhitaji maalum kiitwacho African Genius Foundation, Tawi la Songwe.

Nyamakomago alisisitiza suala la malezi bora kwa wajukuu wanaoishi na wazee na kuwataka wazee hao kuwafundisha mila na desturi za kitanzania ili kuzuia mmomonyoko wa maadili kwa watoto kwa lengo la kujenga taifa imara linalokemea na kupinga vitendo vya ukatili na uhalifu kwa maendeleo ya nchi.

Aliwaomba wananchi wa Mkoa wa Songwe kuendelea kutoa msaada kwa watu wenye uhitaji maalum kama kilivyofanya kikundi cha African Genius Foundation kwa kuwa kufanya hivyo ni neema kwa Mwenyezi Mungu.

Mhamasishaji na Mratibu wa kikundi hicho Mkoa wa Songwe, Mkaguzi Msaidizi wa Polisi, Sadam Kitembe, alisema wamejiwekea utaratibu wa kuwasaidia watu wenye uhitaji maalum kama vile yatima, wajane, wazee na watu wanaoishi katika mazingira magumu kwa lengo la kuwaweka karibu na jamii.

Wazee hao walishukuru Jeshi la Polisi Mkoa wa Songwe kwa elimu waliyoipata, wakiahidi kutoa ushirikiano katika kila jambo linalohusu uhalifu na ukatili wa kijinsia na unyanyasaji dhidi ya watoto ili kuwa na jamii bora iliyo na kizazi imara.

Katika hafla hiyo, wazee hao walipata nafasi ya kushiriki chakula cha mchana na viongozi wa kikundi hicho na kupatiwa mahitaji mbalimbali kama sabuni, mchele, mafuta ya kupikia, mafuta ya kupakaa, sukari, chumvi na mavazi.



Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria wakiwa katika kikao jana jijini Dodoma. **PICHA: BUNGE**

# Mkakati kuinua ufaulu somo la Hisabati wapata ufadhili

**Na Halfani Chusi**

KATIKA kuongeza ufaulu kwenye somo la Hisabati, Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) imefadhili mpango wa kuchochea kiu ya kufundisha na kujifunza somo hilo katika Jimbo la Ubungo, Dar es Salaam unaofahamika kama KiuHisabati.

Mpango huo ulioasisiwa na Mbunge wa Ubungo, Prof. Kitila Mkumbo, unalenga kuongeza ufaulu kwenye somo hilo kupitia motisha ya tuzo na zawadi ya fedha kwa walimu wanaofaulisha wanafunzi kwenye somo hilo.

Pia unalenga kuwafadhili wanafunzi waliofanya vizuri katika somo hilo pale wanapofaulu kwenda kidato cha tano kwa shule za sekondari.

Hafla ya utoaji tuzo hizo kwa walimu hao ilifanyika mwishoni mwa wiki jimboni huko, ikiongozwa na Naibu Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Bara ambaye ni Kaimu Katibu Mkuu wa chama hicho, Anamringi Macha.

Pia ilihudhuriwa na viongozi waandamizi wa chama na serikali Mkoa wa Dar es Salaam, walimu, wananchi na maofisa wa Benki ya NBC wakiongozwa na Meneja wa Benki hiyo Tawi la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Anne Mwaisaka.

Baada ya hatua hiyo, Macha alimpongeza mbunge huyo kwa kubuni mpango huo akiishukuru na kuiomba Benki ya NBC iangalie namna inavyoweza kutanua mpango huo kufika maeneo mbalimbali nchini ili uwanufaishe walimu na wanafunzi wengi zaidi, hatua ambayo alisema itasaidia kuchochea kasi ya ufaulu wa somo hilo.

"Hesabu ndio nguzo mama ya masomo yote, kwenye mfumo wa elimu yetu. Jitihada zozote zinazofanywa na wadau mbalimbali kuongeza ufaulu kwenye somo hili zinaungwa mkono na chama pamoja na serikali kwa ujumla.

"Hii ndio sababu tunampongeza Mbunge wa Ubungo kwa ubunifu huu mzuri na zaidi pia tuishukuru Benki ya NBC kwa ufadhili wake kwenye mpango huu... tunaomba sana NBC mwangalie namna ya kutanua zaidi mpango huu," alisema Macha.

Akifafanua zaidi kuhusu mpango huo, Prof. Mkumbo, mbali na kushukuru Benki ya NBC kuwa mfadhili mkuu wa mpango huo, pia alisema unahusisha walimu na wanafunzi watakaopata daraja A katika somo la Hisabati na wanafunzi watakaofaulu somo hilo kwa kiwango cha daraja A na B.

"Kila mwalimu wa somo la Hisabati atapata Sh. 100,000 kwa kila mwanafunzi atakayepata daraja A katika matokeo ya mtihani wa taifa wa kidato cha nne katika somo hilo.

"Mwanafunzi atakayepata daraja A katika matokeo ya mtihani wa taifa wa kidato cha nne katika somo la Hisabati atanunuliwa vifaa vyote muhimu vya shule, ikiwamo sare, madaftari na vitabu kama atajiunga na shule ya serikali kidato cha tano," alifafanua.

Alisema tangu kuanza kwa mpango huo mwaka 2020, tathmini inaonesha kuwa kumekuwa na ongezeko la idadi ya wanafunzi wanaopata alama A na B katika jimbo hilo, lakini si katika kupunguza idadi ya wanafunzi wanaofeli somo la Hisabati.

"Hii inaonesha kuwa programu ya motisha kwa walimu imekuwa na tija katika kuwahamasisha wanafunzi kujifunza zaidi hisabati.

"Hata hivyo, changamoto bado ni kubwa kwa kuzingatia takwimu kwamba wastani wa ufaulu kwenye somo hili kwa jimbo hili la Ubungo ni asilimia 11 tu huku wastani wa ufaulu kitaifa kwa somo hili ukiwa ni asilimia 19 hadi 20," alisema.

Meneja wa NBC Tawi la UDSM, Anne Mwaisaka, alisema hatua ya benki hiyo kufadhili mpango huo ni mwendelezo wa jitihada za taasisi hiyo kuunga mkono mipango ya serikali pamoja na wadau mbalimbali yenye nia ya kuboresha sekta ya elimu nchini.

"Kimsingi, ufadhili wetu kwenye mpango huu unalenga kuchochea utoaji wa motisha kwa walimu na wanafunzi waliofanya vizuri kwenye somo la Hisabati katika mtihani wa kidato cha nne.

"Tukiwa kama taasisi ya fedha, moja kwa moja tunakuwa wadau wa elimu likiwamo somo la Hisabati kwa kuwa shughuli zetu kwa kiasi kikubwa zinaongozwa na hesabu, hivyo tuna wajibu pia wa kuhakikisha ustawi wake," alisema.

Akitoa shukrani zake kwa niaba ya walimu na wanafunzi walionufaika na mpango huo, Mwalimu Michael Msembwe kutoka Shule ya Sekondari Kimara ambaye aliongoza kwa kufaulisha wanafunzi 20 kwa ufaulu wa Daraja A kwenye somo hilo, alisema ujio wa mpango huo umeongeza chachu na motisha kwa walimu na wanafunzi.

# Benki yapongezwa kupata faida bilioni 78/-

**Na Sabato Kasika**

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Riziki Pembe Juma, ameipongeza Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) kwa kupata faida ya Sh. bilioni 78 mwaka jana, hatua itakayosaidia kuipa gawio serikali.

Riziki alisema hayo wakati akifungua tawi la benki hiyo eneo la Nungwi, Wilaya ya Kaskazini A, Unguja jana, ikiwa ni sehemu ya shamrashamra za madhimisho ya Miaka 60 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar.

Alisema mwaka juzi ilishuka kwa kupata faida ya Sh. bilioni 22, lakini pia imetoa mkopo wa Sh. trilioni moja kwa wateja wake na kuendelea kuwa kiungo muhimu ndani ya Zanzibar na Tanzania Bara.

"Mafanikio hayo yanatokana na miongozo ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza Mapinduzi Dk. Hussein Ali Mwinyi, kupitia Wizara ya Fedha na Mipango kwa kusimamia na kujenga vyanzo vingi vya fedha," alisema Riziki.

Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Dk. Juma Malik, alisema, sera na miongozo pamoja na busara ni matokeo ya viongozi wakuu wa nchi mbili yenye lengo la kuwaletea wananchi maendeleo.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa PBZ, Said Mohammed Said, alisema, kimtandao benki hiyo imekua kwa kasi na kwamba mwaka 2020 ilikuwa na matawi 29 huku akifafanua kwa miaka mitatu hadi mwaka jana, kumekuwa na matawi 46, kukiwa na vituo 35 Zanzibar na 11 kwa Tanzania bara.

"Benki ya Watu wa Zanzibar ni taasisi ya kifedha inayomilikiwa na wananchi, pia ni miongoni mwa matunda ya mapinduzi ambayo ilianzishwa ndani ya miaka miwili baada ya Mapinduzi ya Zanzibar, sasa inatimiza miaka 58," alisema Said.

Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Rashid Hadid Rashid, amewataka wakazi wa Nungwi kuitumia benki hiyo kulipia malipo ya serikali, kubadilisha fedha za kigeni na kufungua akaunti kwa kuweka na kutoa fedha, ili kuziweka katika sehemu salama.

Aidha, aliwaomba wafanyakazi wa benki kutoa elimu ya matumizi sahihi ya fedha kwa wajasiriamali, mitaji, masoko na kupunguza masharti ya mkopo ili kuendana na dhamira ya Rais wa Zanzibar ya kutaka wananchi wawe na maendeleo.

# Pakistan yachunguza mauaji ya vinyozi sita yaliyotekelezwa kwa risasi

**PAKISTAN,**

MIILI ya watu sita waliouawa kwa kupigwa risasi iligunduliwa shambani huko North Waziristan, wilaya ya kikabila kaskazini magharibi mwa Pakistan katika jimbo la Khyber Pakhtunkhwa linalopakana na Afghanistan.

Miili ya marehemu hao ilitambuliwa kuwa ni vinyozi kutoka jimbo la mashariki la Punjab, Pakistan.

Akizungumza na idhaa ya Kiurdu ya VOA, Ofisa wa Polisi wa Wilaya Roohan Zeb Khan alieleza kuwa tukio hilo la mauaji hayo ni la kigaidi.

Alisema kuwa mauaji hayo yanachunguzwa na miili hiyo itakabidhiwa kwa familia zao baada ya zoezi la kuwatambua kukamilika.

Haji Mujtaba, mwandishi wa habari katika eneo, alisema vinyozi wote walikuwa na maduka yao katika soko hilohilo huko Mir Ali, mji mkubwa wa pili huko North Waziristan. Alisema watu hao walitekwa siku moja kabla ya tukio hilo.

Hakuna kundi lililodai kuhusika hadi sasa, lakini kuwapo wanamgambo wenye silaha, hususan kutoka katika kundi lililopigwa marufuku la Tehreek-e-Taliban Pakistan, au TTP, umeongezeka kwa kiwango kikubwa katika wilaya mbalimbali za kikabila tangu Taliban ya Afghanistan kurejea madarakani katika upande wa pili wa mpaka Agosti 2021.

Taliban walipoingia madarakani mara ya kwanza Afghanistan kuanzia 1996 hadi 2001, wanaume walipigwa marufuku kunyoa ndevu zao au kukata nywele kuwa fupi au mkato wa mitindo inayovuma. Wale waliokaidi mara nyingi waliadhibiwa kwa kupigwa, huku nywele zao zikinyolewa.

TTP iliweka masharti kama hayo kwa Wapakistani baada ya wanamgambo kuchukua udhibiti wa eneo la bonde la Swat mapema katika miaka ya 2000. Utawala wao wa vitisho ulimalizika baada ya operesheni ya kijeshi kufanyika mwaka 2009.

Vipeperushi viliwakataza vinyozi kuwakata nywele wanaume katika mtindo fulani ambavyo vilionekana katika maeneo ya kikabila ya Pakistan katika miezi kadhaa iliyopita.

Haiko bayana, hata hivyo, iwapo vinyozi sita hao walilengwa kwa kazi yao.

Katika taarifa iliyotumwa kwenye vyombo vya habari jioni, TTP imekanusha kuhusika na tukio hilo. **VOA**

**Alisema kuwa mauaji hayo yanachunguzwa na miili hiyo itakabidhiwa kwa familia zao baada ya zoezi la kuwatambua kukamilika.**




Msemaji wa Jeshi la Israel, Daniel Hagari

# Mauaji ya kiongozi wa Hamas Beirut yazidisha shaka ya vita

**JERUSALEM,** ISRAEL

JESHI la Israel limesema limejiandaa kwa hali yoyote baada ya shambulio mjini Beirut, lililomuua naibu kiongozi wa Hamas na kuchochea hofu ya vita katika Ukanda wa Gaza kugeuka mzozo wa kikanda.

Arouri mwenye umri wa miaka 57, ndiye ofisa wa kwanza wa ngazi ya juu wa Hamas kuuawa tangu Israel ilipoanzisha mashambulizi makubwa ya angani na ardhini dhidi ya kundi hilo karibu miezi mitatu iliyopita, kufuatia uvamizi wa kushtukiza na mashambulizi dhidi ya miji ya Israel.

Israel haijathibitisha wala kukanusha kufanya mauaji ya Arouri, lakini msemaji wa jeshi lake, Daniel Hagari alisema vikosi vya Israel vilikuwa katika hali ya juu ya utayari na vimejindaa kwa hali yoyote.

Israel ilimtuhumu Arouri kwa muda mrefu kuhusika na mashambulizi ya mauaji dhidi ya raia wake, lakini ofisa wa Hamas alisema alikuwa muhimu sana katika majadiliano yaliofanywa na Qatar na Misri juu ya matokeo ya vita vya Gaza na kuachiwa kwa mateka wa Israel walioshikiliwa na Hamas.

Nasser Kanaani, Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje ya Iran, ambayo ni muungaji mkono mkubwa wa Hamas na kundi la Hezbollah la Lebanon, amesema mauaji ya Arouri yatachochea zaidi hamasa ya upinzani na kuongeza motisha katika mapambano dhidi ya wakaliaji wa Kizayuni, si tu katika maeneo ya Wapalestina, bali pia katika kanda nzima na miongoni mwa wapiganiaji uhuru kote duniani.

**UN YAELEZA WASIWASI**

Akizungumza mjini New York jana, baada ya mauaji hayo kuripotiwa, Naibu Msemaji wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Florencia Soto Nino, aliyataja mauaji hayo kuwa kosa la kimahesabu linalosababisha wasiwasi mkubwa na linalotilia mkazo kile ambacho Katibu Mkuu Antonio Guterres amekisema juu ya hatari ya kusambaa kwa mzozo huo katika kanda pana, na kutoa wito wa kujizuia.

"Kwahiyo, tunatoa wito tena kwa wanachama wote wa jumuiya ya kimataifa kufanya kila wawezalo ili kuzuia kuongezeka kwa mzozo huko. Kwa sababu ya mvutano unaozidi na kudorora kwa hali katika kanda, tunatoa wito kwa pande zote kujizuia. Hatutaki kukurupuka kokote, vitendo vyovyote vya kukurupuka ambavyo vinaweza kusababisha vurugu zaidi," alisema Soto Nino.

Mamia ya Wapalestina waliandamana mjini Ramallah na miji mingine katika Ukingo wa Magharibi kulaani mauaji ya Arouri, huku wakipaza sauti za "Kisasi, kisasi, Qassam!" Wakimaanisha tawi la kijeshi la kundi la Hamas, ambalo linapambana na vikosi vya Israel Gaza.

Hofu pia imetawala juu ya hatua gani zitachukuliwa na kundi la Hezbollah, mshirika mkubwa wa Hamas na ambalo kiongozi wake Sayyed Hassan Nassrallah aliweka wazi kwamba hatua yoyote ya Israel kuwalenga viongozi wa Hamas walioko nchini Lebanon itajibiwa vikali.

Serikali ya Lebanon imesema ilikuwa katika mazungumzo na vuguvugu la Hezbollah kuzuia kuongezeka kwa mzozo na Israel.

Kaimu Waziri wa Mambo ya Nje, Abdallah Bou Habib, alikiambia kituo cha BBC cha Uingereza Jumanne usiku, kwamba serikali yake ilikuwa inazungumza na Hezobollah kuwashawishi kutojibu mauaji hayo.

"Tuna wasiwasi sana, (Walebanon) hawataki kuingizwa katika hilo, hata Hezbollah haitaki kuingizwa kwenye vita vya kikanda," alinukuliwa akisema. Wizara ya Mambo ya Nje ya Lebanon ilianza "kutayarisha malalamiko kwa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kulaani uvamizi wa Israel, kwa kuzingatia maagizo ya Waziri Mkuu wa Muda, Najib Mikati," Shirika la Habari la Taifa linaloendeshwa na serikali lilisema.

Kundi lingine la Wahouthi nchini Yemen, ambalo limekuwa linazishambulia meli za kibiashara katika Bahari ya Shamu kushinikiza Israel kuacha kuishambulia Gaza, limesema litazidisha mashambulizi yake na kutishia kuzilenga pia meli za kivita za Marekani ikiwa lenyewe litalengwa.

Jumla ya Wapalestina 22,313 wameuawa na 57,296 wamejeruhiwa katika mashambulizi ya Israel dhidi ya Gaza tangu Oktoba 7, mwaka jana, kwa mujibu wa Wizara ya Afya ya Gaza katika taarifa ya jana.

"Takribani Wapalestina 128 wameuawa na 261 kujeruhiwa katika muda wa saa 24," iliongeza wizara hiyo.

Ujerumani, Marekani, Umoja wa Ulaya na mataifa kadhaa mengine yanaiorodhesha Hamas kama kundi la kigaidi. **DW**

HABARI MICHEZO

# STARS KAMILI KUIVAA MISRI J'PILI

**Na Saada Akida**

KOCHA Msaidizi wa Timu ya Taifa Stars, Hemed Morocco, amesema kikosi kimewasili salama Misri na wamefarijika kuona hali ya utimamu wa mwili wa wachezaji waliopo kambi ikiendelea vizuri katika maandalizi ya Fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) 2023 zinazotarajiwa kuanza Januari 13, mwaka huu.

Kikosi cha Stars kipo nchini Misri kwa siku saba kwa ajili ya kambi na kucheza mechi ya kirafiki dhidi ya Timu ya Taifa ya Misri, Jumapili wiki hii kabla ya kwenda nchini Ivory Coast katika fainali hizo.

Akizungumza na Nipashe jana, Morocco alisema baada ya kuwasili nchini humo wanaendelea na program ya mazoezi kujiandaa na mashindano hayo na tayari wachezaji wawili Himid Mao na Khlefin Hamdoun wamejiunga na wenzao kwa ajili ya maandalizi hayo.

Alisema wanafarijika kuona utimamu wa wachezaji walikuwapo kambini hapo na wanaimani na wachezaji wengine ambao wataungana nao hivi karibuni kwa ajili ya kuendelea na programu za kiufundi kuandaa kikosi kuelekea fainali hizo.

"Tumewasili salama nchini Misri tutakuwapo hapa kwa ajili ya maandalizi kuelekea fainali za AFCON, leo (jana) tuliwasili usiku tukafanya mazoezi na tutacheza dhidi ya Timu ya Taifa ya Misri kabla ya kwenda nchini Ivory Coast ambapo tutaenda kucheza fainali hizo," alisema Morocco.

„Tutakuwa na mechi za kirafiki, moja tutacheza dhidi ya Timu ya Taifa ya Misri kabla ya kwenda nchini Ivory Coast ambapo tutaenda kucheza fainali hizo," alisema Morocco.

Naye Kiungo wa Stars, Himid Mao, alisema hali ya kambi ni nzuri na tayari wameanza maandalizi na anatumai siku zijazo watazidi kuwa vizuri na kutengeneza muunganiko na wachezaji wapya ambao wameungana na kikosi kwa mara ya kwanza.

"Hali ya kambi ni nzuri, mchezaji yeyote ambaye anaungana na wenzake hapa kwa mara ya kwanza kulitumikia taifa letu, tunahitaji msaada mkubwa katika kupambana na kuipeperusha vema bendera ya Tanzania hasa tunapoelekea katika fainali hizi za AFCON," alisema Himid. Aliwaomba Watanzania kuendelea kuwasapoti katika kila hali, kwa kuwa kuunganisha nguvu zao watafanikiwa kwenye malengo ambayo tarajiwa katika fainali hizo.

Stars itaanza kutupa karata yake ya kwanza kwenye fainali hizo Januari 17 dhidi ya Morocco na kisha Januari 21 itavaana na Zambia na baada ya hapo Januari 24, mwaka huu, itahitimisha mchezo wake wa hatua ya makundi dhidi ya DR Congo.

KIKAPU...



Wachezaji wa mpira wa kikapu wa timu ya Vijana, wakifanya mazoezi katika viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# RT yamwahidi Rais Samia makubwa 2024

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Shirikisho la Riadha Tanzania (RT), umeweka wazi kuwa mwaka huu wa 2024 hawatamwangusha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, katika mchezo huo kwa kuwa malengo yao ni kutaka kuona ukiwa wa mafanikio kao.

Akizungumza na Nipashe jana, Kaimu Katibu Mkuu RT, Wakili Jackson Ndaweka, alisema shirikisho hilo linapongeza hotuba ya Rais Samia aliyoitoa katika mkesha wa mwaka mpya, kwa kugusa sekta ya michezo hususan kutambua mchango mkubwa uliotolewa na wanariadha.

Alisema mbali ya kugusa sekta mbalimbali, hakusahau mchezo wa riadha kwa kuchangia mafanikio na kuitangaza vema Tanzania kimataifa kwa mwaka 2023.

„Sisi kama riadha Tanzania tumeguswa sana na hotuba ya rais, tumefarijika sana pale alipotambua mafanikio ya wanariadha wetu; Magdalena Shauri na Alphonce Simbu, tunaahidi kwa huu mwaka tutaendelea kufanya mazuri katika sekta yetu," alisema Wakili Ndaweka na kuongeza;

„Hii itachochea kujituma zaidi na kufanya vizuri kwa vijana wetu na sisi shirikisho tunaahidi kujituma na kujipanga zaidi kwa kushirikiana na Serikali hususan wizara yenye dhamana na michezo, wadhamini na wadau mbalimbali ili kuleta mafanikio makubwa zaidi katika medani ya riadha."

Katika hotuba yake Rais Samia akielezea mafanikio katika sekta ya michezo alisema: „Kwenye sekta ya michezo, pamoja na kuimarisha miundombinu ikiwamo ukarabati Uwanja wa Benjamin Mkapa, mwaka huu tumepata mafanikio mengi ya kujivunia.

„Timu ya Yanga kupata medali ya pili kwenye Kombe la Shirikisho Barani Afrika (CAF Confederation Cup) na binti wa Kitanzania Magdalena Shauri kuwa mshindi wa tatu kwenye mbio za Berlin Marathon na mwanariadha Alphonce Simbu kuwa mshindi wa pili kwenye mbio za Shanghai Marathon."

# 'Demba Ba' rasmi atua Mbeya City

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Mbeya City inayoshiriki Ligi ya Championship, imemsajili straika Mohamed Haji Hamisi maarufu ‚Demba Ba', kutoka Klabu ya Mashujaa kwa ajili ya kukiongezea nguvu kikosi chao katika kipindi hiki cha usajili wa dirisha dogo.

Taarifa iliyotolewa jana mchana na klabu hiyo imeeleza kuwa klabu hiyo pia imesajili kipa wa zamani wa KMC, Sudi Dondola.

Kocha msaidizi wa timu hiyo, Mathias Wandiba, amesema wameongeza wachezaji wachache kwenye sehemu ambazo zilikuwa na mapungufu, hivyo wanaamini sasa watafanya vizuri katika mechi za mzunguko wa pili wa ligi hiyo.

„Karibu Mohamed, mashabiki wa Mbeya City wanasubiri ile shughuli uliyozoea kuifanya ukiwa uwanjani kwa timu yao pendwa," ilisema taarifa hiyo.

Straika huyo amepachikwa jina la ‚Demba Ba,' kutokana na mwili mkubwa, akifananishwa na mshambuliaji wa zamani wa Timu ya Taifa ya Ufaransa mwenye asili ya Senegal, Demba Ba.

# Muumin aanza mwaka mpya na 'Bila Wewe'

**Na Sabato Kasika**

MWIMBAJI nyota wa Muziki wa Dansi, Mwinjuma Muumin, amefyatua wimbo mpya uitwao ‚Bila Wewe' ikiwa ni maandalizi ya albamu ya kwanza kwa mwaka mpya wa 2024.

Akizungumza na gazeti hili jana, Muumin ambaye kwa sasa amehamishia maskani jijini Mwanza akiwa na kundi lake la Special Band, amesema wimbo huo ulirekodiwa jijini humo wiki iliyopita.

„Ni wimbo ambao umepigwa katika mtindo wa rhumba, unaelezea mapenzi yenye visa vya kweli ambavyo watu wamekuwa wakikutana navyo kwenye mahusiano," alisema Muumin. Alifafanua kuwa katika wimbo huo, moja ya visa vinavyoelezewa ni cha yeye (Muumin) kuporwa mke na mlinzi wa Kimasai na kwamba wimbo umejaa simulizi za kweli.

„Mimi na wanamuziki wangu wakiwamo wapiga vyombo kama Rashid Sumuni (solo), Hosea Mgohachi (besi) na wengine wengi, tumeamua kuhamia Mwanza kuendelea na maisha ya muziki," alisema.

Nyota huyo wa muziki wa dansi, amesema kwa sasa karibu maeneo yote ya nchi muziki huo una mashabiki wengi, tofauti na zamani bendi nyingi zilikuwa zimejichimbia Dar es Salaam.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**PHILLIPS HAKIELEWEKI**

UHAMISHO wa kiungo wa kati wa Manchester City na England, Kalvin Phillips mwenye umri wa miaka 28, kwenda Newcastle United unaweza usifanyike. Lakini Fulham na Crystal Palace zinavutiwa na mchezaji huyo wa zamani wa Leeds United. **(I Sport)**

**UNITED YAANDAA ORODHA**

KLABU ya Manchester United imeandaa orodha ya wachezaji wanne ili kupata mshambuliaji mpya Januari, ambaye ni Mcameroon wa Bayern Munich, Eric Maxim Choupo-Moting mwenye umri wa miaka 34, Thomas Muller (34). Klabu hiyo pia imewasiliana na RB Leipzig juu ya Timo Werner wa Ujerumani mwenye miaka 27 na mshambuliaji wa Stuttgart na Guinea, Serhou Guirassy, 27. **(Athletic)**

**TONEY KUHAMIA ARSENAL**

MSHAMBULIAJI wa England, Ivan Toney mwenye umri wa miaka 27, ana matumaini ya kuhamia Arsenal Januari, lakini ‚Washikabunduki' hao hawana nia ya kulipa pauni milioni 100 ambayo Brentford wanaitaka. **(Football Transfers)**

**SPURS NA GALLAGHER**

KLABU ya Tottenham Hotspur haina mpango wa kumnunua kiungo wa kati wa England, Conor Gallagher mwenye umri wa miaka 23, katika dirisha la Januari kwa sababu hawawezi kutimiza matakwa ya Chelsea ya pauni milioni 60 kutokana na vikwazo vya kifedha. **(Football Transfers)**

**LINGARD MKATABA MPYA**

KLABU ya Everton inafikiria kumpa kiungo wa zamani wa Manchester United na England, Jesse Lingard, mkataba hadi mwishoni mwa msimu huu. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, kwa sasa yupo huru. **(Talksport)**

**DURAN ANALENGWA**

MSHAMBULIAJI wa Aston Villa na Colombia, Jhon Duran mwenye umri wa miaka 20, analengwa na AC Milan ya Italia. **(Sky Sports)**

**COUFAL HAJAFURAHISHWA**

MLINZI wa West Ham na Jamhuri ya Czech, Vladimir Coufal mwenye umri wa miaka 31, hajafurahishwa na mkataba wake na anataka klabu hiyo imwache aondoke katika dirisha la uhamisho la Januari ikiwa hatopewa mkataba mzuri. **(Sky Sports)**

**TOMIYASU MKATABA MPYA**

ARSENAL imeanza mazungumzo juu ya mkataba mpya kwa mlinzi wao raia wa Japan, Takehiro Tomiyasu, 25. **(Mail)**

**KALAJDZIC ALENGWA**

MSHAMBULIAJI wa Wolves na Austria, Sasa Kalajdzic mwenye umri wa miaka 26, analengwa na Eintracht Frankfurt, huku klabu hiyo ya Ujerumani ikisubiri kuona kama Gary O'Neill ataidhinisha uhamisho wa mkopo. **(Mail)**

**ANDRE BASI TENA FULHAM**

MPANGO wa Fulham kumnunua kiungo wa kati wa Fluminense na Brazil, Andre mwenye umri wa miaka 22, umesitishwa kwa sababu hawataki kufika bei inayotakiwa ya pauni milioni 25. Na sasa wanaamini kiungo wa kati wa Ureno, Joao Palhinha mwenye umri wa miaka 28, atasalia katika klabu hiyo. **(Football Transfers)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MSHAHARA WA SANCHO KIGINGI KUONDOKA UTD

●●● Dortmund wameitaka klabu hiyo wawe wanamlipa mshahara kiasi cha theluthi mbili, lakini...

**MANCHESTER, England**

MANCHESTER United na Borussia Dortmund zipo kwenye mazungumzo juu ya mkataba wa mkopo wa Jadon Sancho, kwa mujibu wa ESPN.

Dortmund inataka kumsajili Sancho hadi mwishoni mwa msimu huu, lakini inaitaka United kuendelea kulipa sehemu kubwa ya mshahara wake.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, hajaichezea United tangu Agosti kutokana na mabishano ya hadharani na Kocha Erik ten Hag.

Fowadi huyo wa England amefukuzwa kwenye kikosi cha kwanza kwa miezi minne na amelazimika kufanya mazoezi peke yake chini ya uangalizi wa wafanyakazi wa klabu hiyo.

Sancho pia amezivutia Juventus na RB Leipzig, lakini kwa mujibu wa ESPN yeye anapendelea zaidi kujiunga na klabu yake ya zamani ya Dortmund.

Aliondoka Dortmund na kusajiliwa na United mwaka 2021 kwa mkataba wa thamani ya pauni milioni 73. Mabosi wa United wamekubali kwamba kuna matarajio madogo ya Sancho kuwa na mustakabali Old Trafford huku Ten Hag akiwa kocha, lakini klabu hiyo ina nia ya kupunguza gharama za kuondoka kwake.

Mshahara wa Sancho wa zaidi ya pauni 300,000 kwa wiki ni mkubwa kwa klabu nyingi za Ulaya ikiwa ni pamoja na Dortmund na United wanataka kutoa sehemu tu ya mshahara wake.

United ilikubali mkataba wa mkopo na Eintracht Frankfurt kwa Donny van de Beek ambapo timu hiyo ya Ujerumani ilichukua sehemu kubwa ya mshahara wa kiungo huyo, lakini kwa Sancho Dortmund wanataka United kulipa kiasi cha theluthi mbili.

Mechi ya mwisho ya Sancho kwa United ilikuwa ni ile ya ushindi wa mabao 3-2 dhidi ya Nottingham Forest Agosti 26, mwaka jana.

Aliondolewa kwenye kikosi kilichofungwa 3-1 na Arsenal Septemba 3, mwaka jana na baadaye akatoa taarifa kwenye mtandao wa kijamii akipinga sababu iliyotolewa na Ten Hag kwamba alikuwa hajitumi mazoezini.

Ten Hag ametaka kuombwa radhi kwa faragha na hadharani kabla ya kumruhusu Sancho kurejea kikosini, jambo ambalo hadi sasa mshambuliaji huyo amekataa kulifanya.




# ROONEY AGEUKA FUNGU LA KUKOSA KWENYE UKOCHA

**BIRMINGHAM, England**

WAYNE Rooney amefukuzwa kazi ya ukocha Birmingham City baada ya kufungwa mara tisa katika mechi 15 na kuiacha timu hiyo ukingoni mwa eneo la kushuka daraja la michuano ya Championship.

Wamiliki wa Birmingham kutoka Marekani, Knighthead Capital Management, wakiongozwa na mwanzilishi mwenza wa Kampuni, Tom Wagner, walimwondoa Rooney kutoka wadhifa wake Jumanne baada ya kichapo cha 3-0 kutoka kwa Leeds United siku ya mwaka mpya.

Katika taarifa iliyotolewa Jumanne, Birmingham ilisema: "Birmingham City leo (juzi) imeachana na kocha Wayne Rooney na kocha wa kikosi cha kwanza, Carl Robinson.

"Pamoja na jitihada zao nzuri, matokeo hayajakidhi matarajio ambayo yaliwekwa wazi hapo awali. Kwa hiyo, Bodi inahisi kuwa mabadiliko ya usimamizi ni kwa manufaa ya klabu."

Klabu hiyo iliwashukuru Rooney na Robinson kwa muda wao na kusema kocha wa maendeleo ya kitaaluma, Steve Spooner atachukua jukumu la kuifundisha klabu hiyo kwa muda.

Vyanzo viliiambia ESPN kwamba nafasi ya Garry Cook, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Birmingham, ambaye alimwajiri Rooney, pia inachunguzwa.

"Kwa bahati mbaya, wakati wa Wayne na sisi haukwenda kama ilivyopangwa na tumeamua kuelekea katika mwelekeo tofauti," alisema Cook katika taarifa ya Birmingham.

Mshambuliaji huyo wa zamani wa Manchester United na England, Rooney, ambaye aliacha kazi yake kama kocha wa Klabu ya Ligi Kuu ya Soka Marekani (MLS), D.C. United na kuchukua mikoba ya Birmingham Oktoba, aliimbiwa nyimbo za "unafukuzwa asubuhi" na mashabiki wa timu yake huko Leeds.

Akiwa amerithi timu kutoka kwa mtangulizi wake, John Eustace, ambaye alifukuzwa kazi Oktoba, Rooney alitia saini mkataba wa miaka mitatu na nusu katika klabu hiyo ya St Andrew na kuahidi kuleta "bila hofu" soka katika klabu hiyo.

Lakini Rooney mwenye umri wa miaka 38, alipokea kichapo mara nne katika mechi zake tano za kwanza na kuifanya Birmingham kuporomoka kwenye jedwali.

# Ancelotti: Madrid haitasajili mlinzi

**MADRID, Hispania**

KOCHA Carlo Ancelotti amekataa kusajili beki mwezi huu, akiunga mkono kikosi kilichopo cha Real Madrid kukabiliana na kukosekana kwa beki wa kati chaguo la kwanza akishirikiana na Eder Militao na David Alaba.

Militao amekuwa nje ya uwanja kwa muda mrefu tangu Agosti kutokana na kupasuka kwa msuli wa paja, huku Alaba alipata jeraha hilo hilo katika ushindi wa 4-1 wa Madrid dhidi ya Villarreal Desemba 17, mwaka jana.

Kabla ya Krismasi, Ancelotti alisema kwamba klabu ingefikiria kusajili katika dirisha la uhamisho la Januari, lakini kocha huyo raia wa Italia - ambaye alitia saini mkataba mpya wa miaka miwili wiki iliyopita - alipuuzia uwezekano huo Jumanne.

"Kwa wakati huu, hatufikirii kusajili beki mwingine wa kati," alisema Ancelotti katika mkutano na waandishi wa habari kabla ya mchezo wa kwanza wa Madrid mwaka 2024, dhidi ya Real Mallorca kwenye LaLiga.

"Tunakosa wachezaji muhimu, lakini tunao wengine wawili ambao tunawaamini, Nacho (Fernandez) na (Antonio) Rudiger, na wengine wawili ambao wanaweza kucheza, (Aurelien) Tchouameni na (Dani) Carvajal."

Ancelotti alikataa kushughulikia uvumi kwamba Madrid itaanzisha mazungumzo mwezi huu na Kylian Mbappe - ambaye sasa yuko huru kufanya mazungumzo baada ya kuingia miezi sita iliyopita ya mkataba wake na Paris Saint-Germain - akisema "Sitagusa suala hilo," na alisema kikosi cha Madrid kitahitaji kuongezewa nguvu kidogo msimu ujao wa majira ya joto.

"Kwanza kuna wachezaji ambao mikataba yao imeisha, watachagua wanachotaka kufanya," alisema.

"Namzungumzia (Toni) Kroos, Nacho, Luka Modric. Yajayo tayari yameandikwa, hakuna mengi ya kufanya. Timu hii tayari inaelekea katika mwelekeo sahihi, ikiwa na wachezaji wachanga wanaovutia sana."

Madrid ilitangaza mkataba mpya wa Ancelotti hadi Juni 2026 Ijumaa iliyopita baada ya uvumi wa mara kwa mara wa kumhusisha na Timu ya Taifa ya Brazil.

"Ukweli ndio kila mtu anajua," Ancelotti alisema Jumanne. "Niliwasiliana na rais wa zamani wa Shirikisho la Brazil, Ednaldo Rodrigues. Nataka kumshukuru kwa mapenzi na nia, ilinifanya nijivunie sana, lakini kilicho wazi kwa kila mtu inategemea hali yangu ndani ya Real Madrid."

# Wakala wa Ziyech kurejea Chelsea

**MADRID, Hispania**

WAKALA aliyehusika na kukamilisha uhamisho wa mkopo wa Hakim Ziyech kwenda Galatasaray kutoka Chelsea, amekanusha madai kwamba ameomba mkataba huo ukatishwe mwezi huu.

Ziyech alipata uhamisho wa mkopo msimu uliopita, huku Galatasaray ikithibitisha kuwa hawajalipa ada ya mpango huo na pia walikuwa wamejadiliana haki ya kumsajili Ziyech kwa uhamisho wa bure msimu ujao wa majira ya joto.

Ripoti kutoka Kituo cha Uturuki cha DHA, imesema kwamba Galatasaray inaweza kutarajia kusitisha mkopo mwezi huu huku kukiwa na wasiwasi juu ya pato la Ziyech, na uvumi huo ulichochewa zaidi wakati nukuu zilianza kuibuka kwenye mitandao ya kijamii ambayo inadaiwa ilionesha wakala George Gardi akithibitisha Galatasaray itapunguza mpango mfupi.

Akipeleka kwenye mitandao ya kijamii kufafanua hali hiyo, Gardi alizitaja nukuu hizo kama "habari za uwongo".

"Sijawahi kutoa tamko lolote kuhusu Ziyech na sijui mtu huyu ambaye aliandika kwa kutumia jina langu," Gardi aliongeza.

Ziyech mwenye umri wa miaka 30, ameichezea Galatasaray mechi 14 msimu huu, akipachika mabao manne na kutoa pasi mbili za mabao katika michuano yote kabla ya kutinga kwenye Kombe la Mataifa ya Afrika akiwa na Morocco.

Winga huyo bado ana mkataba na Chelsea hadi 2025, lakini kuna uwezekano mkubwa wa kurejea kwenye kikosi kipya cha kocha Mauricio Pochettino iwapo Galatasaray itakataa kumsajili bila malipo mwishoni mwa msimu huu.



Mechi ya mwisho ya Ziyech Chelsea ilikuwa Mei 2023, alipotoa pasi kwenye ushindi wa mabao 4-1 dhidi ya Manchester United akitokea benchi chini ya Kocha Frank Lampard.

HABARI MICHEZO

# AZAM FC YATINGA ROBO FAINALI MAPINDUZI CUP, VITAL'O YAAGA

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

WAKATI Azam FC ikifanikiwa kutinga hatua ya robo fainali ya michuano ya Kombe la Mapinduzi baada ya juzi Jumanne kutoka na ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Vital'O, wapinzani wao hao wameyaaga mashindano hayo.

Azam FC imefikisha alama saba katika michezo mitatu iliyocheza ambapo imeshinda miwili na imetoka sare mchezo mmoja.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kumalizika mchezo wao dhidi ya Vital' O, Kocha Msaidizi wa Azam FC, Yusuph Dabo, aliwapongeza wachezaji wake kwa jitihada kubwa walizoonesha na kufanikiwa kusonga mbele katika michuano hiyo.

Alisema haikuwa kazi rahisi bali ni jitihada na hamasa waliyonayo wachezaji wao kuona kuwa wanafanya vizuri na kufanikisha malengo yao.

Alisema michezo yote waliyocheza ilikuwa migumu na wachezaji walijitahidi kuhakikisha wanafuata maelekezo ya benchi la ufundi ili kuvuka hatua ya makundi na lengo hilo limefanikiwa.

"Michezo migumu na tunaenda katika hatua ngumu, timu ilionesha kujituma kwa hali ya juu ili kupata matokeo ya kusonga mbele na hili tumefanikiwa,"alisema.

Aidha, alisema hivi sasa anakiandaa kikosi chake kuelekea hatua ya robo fainali ya michuano hiyo ili wafanikiwe kutinga hatua ya nusu fainali na hata fainali.

Alisema katika mashindano kila hatua unayopiga inakuwa ngumu hivyo lazima wahakikishe wanayafanyia kazi mapungufu yote ambayo wameyaona katika michezo iliyopita.

Azama FC ipo Kundi A pamoja na timu za Vital'O ambayo rasmi imeaga mashindano, Mlandege FC pamoja na Chipukizi FC.

Katika kundi hilo umebaki mchezo mmoja kati ya Mlandege FC yenye alama mbili dhidi ya Chipukizi ambayo ina pointi moja, hivyo timu itakayofanikiwa kushinda mchezo huo itaungana na Azam FC hatua ya robo fainali.

WAZIRI...



Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro (katikati) na Balozi wa India hapa nchini, Biyana Predhan (kushoto), wakimsikiliza mwanariadha maarufu kutoka India, Milind Soman, wakati wa hafla ya kutoa zawadi kwa wakimbiaji walioshiriki mbio za kirafiki kati ya Tanzania na India jijini Dar es Salaam wiki iliyopita.
**PICHA: JUMANNE JUMA**

# Simba Queens yaifunza soka Yanga Princess

Na Adam Fungamwango

MABAO mawili ya haraka haraka yaliyofungwa na Aisha Mnunka, yameiwezesha Simba Queens kuibuka na ushindi 3-1 dhidi mahasimu wao wa jadi, Yanga Princess katika mechi ya raundi ya tatu ya Ligi Kuu ya Soka Wanawake iliyochezwa jana, Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi, Dar es Salaam.

Ushindi huo umeifanya Simba kufikisha pointi tisa, lakini ikibaki nafasi ya pili nyuma ya JKT Queens ambayo pia ina alama kama hizo, lakini ikiwa na idadi kubwa ya mabao ya kufunga, baada ya juzi kuitandika Amani Queens 10-0, mechi ikichezwa Uwanja wa Ilulu, Lindi.

Wakati Simba ikifikisha mabao 13 baada ya mechi ya jana, JKT Queens ina mabao 15, ikiwa kileleni mwa msimamo.

Winga wa kulia raia wa Kenya, Elizabeth Wambui jana alikuwa nyota wa mchezo, baada ya kutoa 'assist' ya mabao yote matatu.

Aisha alianza biashara mapema tu dakika ya pili akipachika bao la kwanza kwa upande wa Simba, akiunganisha krosi ya Wambui.

Dakika nane baadaye alitumbukia tena wavuni, akifunga bao kwa mtindo wa 'tik-tak' baada ya kazi kubwa iliyofanywa tena na Wambui.

Winga huyo aliondoka na mpira kwenye wingi ya kushoto na kumtoka Diana Antwi, kabla ya kumimina krosi ya juu ambayo kipa raia wa Ghana, Safiatu Salifu, alishindwa kuupangua vema, ukamkuta mfungaji ambaye alijipindua na kupiga 'tik tak' mpira ukajaa wavuni huku kipa akiwa ametoka langoni.

Lilikuwa ni bao la tano kwa Mnunka kwenye Ligi Kuu ya Soka Wanawake msimu huu, akiwa sasa anaongoza kwenye orodha ya wafungaji.

Yanga Pricess ilifanikiwa kupata bao la kwanza dakika nne baada ya kufungwa bao la pili, kutokana na makosa ya kipa wa Simba Queens, Caroline Rufa.

Kipa huyo raia wa Kenya alitoka langoni kuufuata mpira wa faulo uliopigwa na Mnigeria Precious Christopha, lakini hakuupata na lango likawa tupu, hivyo kutompa tabu sana, Neema Paul kuukwamisha wavuni kwa kichwa.

Lilikuwa ni shambulio pekee la Yanga Princess kipindi chote cha kwanza ambalo lilizaa bao, lakini haikufanya lingine lolote la hatari hadi timu zinakwenda mapumziko, huku Simba Queens ikikaribia kufunga mara mbili kupitia kwa Mrundi, Aisha Djaffar dakika ya 34 na Wambui sekunde chache kabla ya kwenda mapumziko.

Dakika nne tu baada ya mapumziko, Mkenya Vivian Corazone, aliiandikia Simba Queens bao la tatu, akiunganisha kwa kichwa krosi nyingine ikitoka winga wa kulia, Wambui.

Yanga Princess ilifanya mabadiliko mengi ya wachezaji kipindi cha kwanza, Simba Queens ikiyafanya kipindi cha pili.

Mfungaji wa mabao hayo mawili, Aisha alifanyiwa madhambi dakika sita kabla ya mechi kumalizika na kulazimika kutolewa nje, nafasi yake ikichukuliwa na Olaiya Barakat.

Matokeo hayo yanaifanya Yanga Princess kubakia na pointi sita, ikipoteza mechi yake ya kwanza ya Ligi Kuu msimu huu.

## Gamondi sasa hatanii, alitaka Mapinduzi Cup

INATOKA UK. 24

Ushindi wa juzi wa Yanga unawafanya kufikisha pointi sita na magoli saba ya kufunga na kuongoza kundi lao ikifuatiwa na KVZ yenye pointi nne, Jamus yenyewe ina pointi mbili huku Jamhuri ikiburuza mkia kwa pointi yake moja.

Yanga ni kama tayari imekata tiketi ya kutinga hatua ya robo fainali ya michuano hiyo inayotarajiwa kumalizika Januari 13, mwaka huu.

Katika hatua nyingine, Klabu ya Yanga imesema wachezaji wao ambao hawajaonekana kwenye michuano ya Kombe la Mapinduzi, Khalid Aucho, Yao Kouassi, Pacome Zouzoua na Salum Abboubakar 'Sure Boy', wanatarajiwa kuungana na kikosi hicho kwa ajili ya mechi za nusu fainali.

Akizungumza jana kutoka mjini Zanzibar, Makamu wa rais wa klabu hiyo, Arafat Haji, alisema baada ya timu hiyo kutinga hatua ya robo fainali kwa kuichapa Jamus FC ya Sudan Kusini mabao 2-1, wachezaji wao wanatarajiwa kuungana na wenzao baada ya kumaliza muda wao wa mapumziko waliopewa.

„Nimeridhishwa na kiwango cha vijana jinsi walivyocheza, tumesonga mbele kwenye hatua inayofuata, tunakwenda kujipanga na mechi nyingine dhidi ya KVZ ili tushinde bila ya kutia doa katika mpangilio wetu wa kulichukua kombe hili na ushindi huo umetufanya kuwa na uhakika wa kutinga hatua hiyo bila ya kusubiri mechi ya mwisho, na kwa sababu tayari tuna tiketi hiyo mkononi wale wachezaji wetu ambao tuliwapa mapumziko wataungana na kikosi hicho kwa ajili ya mechi zinazofuata.

„Tuna Khalid Aucho, Yao Kouassi, Pacome Zouzoua, Salum Aboubakar 'Sure Boy', na wao muda wao wa mapumziko waliopangiwa unaisha na timu tayari imeshasonga mbele na wao watakuwapo mtawaona pamoja na Hafiz Konkoni," alisema Makamu huyo.

Awali kulikuwa na tetesi kuwa Konkoni alirejea Dar es Salaam kwa ajili ya matayarisho ya safari ya kwenda nchini Ghana kujiunga na Bechem United, timu aliyotoka Augustine Okra ikisemekana kuwa ni moja kati ya makubaliano ya kumsajili mchezaji huyo.

## Kramo arejea, watatu wapya waja Simba

INATOKA UK. 24

fanyika usiopungua wachezaji watatu.

„Mashabiki wa Simba wanatakiwa kuwa na subira kwa sababu viongozi wanaendelea na mchakato wote wa usajili kulingana na mahitaji ya benchi la ufundi na tunatarajia kushusha vifaa vipya," alisema Ahmed.

# Michezo


Alhamisi Januari 4, 2024

Nipashe


## Mshahara wa Sancho kigingi kuondoka Utd

UKURASA 21





## Simba Queens yaifunza soka Yanga Princess

Winga wa Simba Queens, Elizabeth Wambui, akimtoka beki wa Yanga Princess, Diana Antwi kwenye mechi ya Ligi Kuu ya Soka ya Wanawake iliyopigwa Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam jana. Simba Queens ilishinda 3-1. **MPIGAPICHA WETU**

UKURASA 23

# GAMONDI SASA HATANII, ALITAKA MAPINDUZI CUP

●●● Pacome, Yao, Aucho waitwa Z'bar kuiongezea nguvu robo fainali, asema...

**Faustine Feliciane, Z'BAR na Adam Fungamwango, DAR**

LICHA ya ushindi wa mabao 2-1 walioupata juzi usiku dhidi ya Jamus ya Sudan Kusini, Kocha wa Yanga, Miguel Gamondi, amekiri baadhi ya wachezaji wake hawakuwa na mchezo mzuri lakini akisifu ubora wa wapinzani wao kwenye kujilinda huku akisema wanalitaka taji hilo.

Yanga juzi iliwabidi wasubiri mpaka dakika za majeruhi kuweza kupata ushindi wao wa pili kwa michuano ya Mapinduzi shukurani kwa bao la Nickson Kibabage aliyefunga la ushindi.

Akizungumza baada ya mchezo huo, Gamondi alisema walijitahidi kumiliki mpira, lakini walishindwa kutengeneza nafasi kutokana na uimara wa safu ya ulinzi ya wapinzani wao.

„Najaribu kuwapa nafasi wachezaji ambao wanakosa nafasi kwenye kikosi cha kwanza, tumejitahidi kumiliki mpira, lakini hatukuweza kutengeneza nafasi... ndio mpira ulivyo muda mwingine unakuwa na wakati mgumu uwanjani," alisema Gamondi.

Aidha, alisema kwenye mashindano hayo ya Mapinduzi anafanya kile ambacho mashabiki wa timu walikuwa wakikipigia kelele juu ya mzunguko wa wachezaji kwenye kupata nafasi ya kucheza.

„Nadhani mashabiki wanaona namna wachezaji wanavyopata nafasi ya kucheza... mashindano haya nataka kupata fursa ya kuwatumia zaidi wale ambao walikuwa hawapati nafasi kwenye michezo ya ligi na ile ya kimataifa," alisema Gamondi.

Alisema pamoja kuwa wanataka kutwaa ubingwa wa michuano ya mwaka huu, lakini kama kocha anatumia michuano hiyo kuijenga zaidi timu yake na kuwapa nafasi ya kucheza na kutoa mbinu zake kwa wachezaji vijana na wale ambao walikuwa hawapati nafasi.

INAENDELEA UK. 23

# Kramo arejea, watatu wapya waja Simba

**Na Saada Akida**

KIUNGO wa Simba ambaye alikuwa majeruhi kwa muda mrefu, Aubin Kramo, amerejea nchini akiwa fiti na kujiunga moja kwa moja na kikosi cha timu kilichopo Zanzibar kwenye mashindano ya Kombe la Mapinduzi, huku klabu hiyo pia ikitarajia kutambulisha nyota wapya watatu ndani ya wiki hii.

Mbali na Kramo pia kuna nyota mpya ametua nchini juzi usiku na jana kuelekea visiwani Zanzibar kuungana na kikosi cha Simba kilichopo visiwani humo katika mashindano ya Kombe la Mapinduzi yanayoendelea.

Akizungumza na Nipashe jana, Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally, alisema Kramo ametua nchini na kujiunga na timu na atakuwa chini ya uangalizi wa madaktari wa timu.

Alisema kabla hajatua nchini alikuwa akifanya mazoezi mepesi na sasa madaktari wa Simba watamwangalia kwanza kisha kutoa taarifa juu ya kuwa tayari kucheza mechi za ushindani au bado anatakiwa kupewa muda zaidi.

Kuhusu usajili wa dirisha dogo, Ahmed alisema: "Baada ya kumtambulisha kiungo Salehe Karabaka kutoka JKU FC, ni kama rasharasha kwenye mvua, kuna usajili mkubwa unaendelea ku-

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >